
Ripoti ya ufuatiliaji wa malengo ya EFA duniani 2012

2012

ELIMU KWA WOTE



# VIJANA NA STADI

## Kuiweka elimu kwa vitendo



MUHTASARI



United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization

# VIJANA NA STADI
## Kuiweka Elimu Kwa Vitendo

# MUHTASARI

UNESCO Publishing

United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

Ripoti hii ni chapisho huru liliandikwa na UNESCO kwa niaba ya jumuiya ya kimataifa. Ni zao la juhudi za pamoja zilizojumuisha wajumbe wa Timu ya kuandika Ripoti na wadau wengine wengi, asasi, taasisi na serikali

Uteuzi wa wafanyakazi na uwasilishaji wa yaliyomo kwenye chapisho hili hauonyeshi kwa namna yoyote msimamo wa UNESCO kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, mji eneo au mamlaka yake au kuhusiana na mipaka yake

Timu ya kuandika ripoti ya ufuatiliaji wa maelengo ya elimu kwa wote duniani inahusika na uchaguzi na uwasilishaji wa taarifa zilizo kwenye kitabu hiki na misimamo iliyo ndani yake ambayo sio lazima iwe ya UNESCO na ambayo haiifungi Taasisi hii. Kwa jumla Mkurugenzi anawajibika kuhusiana na maoni na misimamo inayoonyeshwa kwenye Ripoti hii

Timu iliyoandika Ripoti ya ufuatiliaji wa malengo EFA duniani

Mkurugenzi: Pauline Rose

Kwame Akyeampong, Manos Antoninis, Madeleine Barry, Nicole Bella, Stuart Cameron, Erin Chemery, Diederick de Jongh, Marcos Delprato, Hans Botnen Eide, Joanna Härmä, Andrew Johnston, Léna Krichewsky, François Leclercq, Elise Legault, Leila Loupis, Alasdair McWilliam, Patrick Montjourides, Karen Moore, Claudine Mukizwa, Judith Randrianatoavina, Kate Redman, Maria Rojnov-Petit, Marisol Sanjines, Martina Simeti, Asma Zubairi.

*Ripoti ya ufuatiliaji wa malengo ya* EFA duniani ni chapisho huru la kila mwaka. Linawezeshwa na kufadhiliwa na UNESCO.

Kwa taarifa zaidi kuhusiana na Ripoti hii, wasiliana na:
EFA Global Monitoring Report team c/o UNESCO, 7, place de Fontenoy
75352 Paris 07 SP, France
Email: efareport@unesco.org
Tel.: +33 1 45 68 07 41
www.efareport.unesco.org

Ripoti zilizopita za EFA
2011. The hidden crisis: Armed conflict and education
2010. Reaching the marginalized
2009. Overcoming inequality: why governance matters
2008. Education for All by 2015 — Will we make it?
2007. Strong foundations — Early childhood care and education
2006. Literacy for life
2005. Education for All — The quality imperative
2003/4. Gender and Education for All — The leap to equality
2002. Education for All — Is the world on track?

Makosa au mapungufu yoyote yaliyogunduliwa baada ya uchapishaji yatarekebishwa kwenye toleo la kwenye mtandao www.efareport.unesco.org.

© UNESCO, 2012
Haki zote zimehifadhiwa
Toleo la kwanza
Limechapishwa 2012 na United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
7, Place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP, France
ED-2012/WS/13
Usanifu wa kompyuta FHI 360
Mpangilio wa ripoti FHI 360

Maktaba ya Congress Cataloging in Publication Data
Takwimu zilizopo
Imepigwa chapa na. UNESCO

*Ukurasa wa kwanza*
© UNESCO/Sarah Wilkins

# Dibaji

Toleo hili la kumi la Ripoti ya ufuatiliaji wa malengo ya EFA duniani halikuweza kwenda na muda. Lengo la tatu la Elimu kwa Wote ni kuhakikisha kwamba vijana wanapata fursa ya kupata stadi. Uharaka wa kufikia lengo hili umeongezeka sana tangu mwaka 2000

Kuanguka kwa uchumi wa dunia kumesababisha ukosefu wa ajira. Kijana mmoja kati nane duniani anatafuta ajira. Idadi ya vijana ni kubwa na inaongezeka. Ustawi na mafanikio yao yanategemea zaidi stadi ambazo elimu na mafunzo yanaweza kuwapa. Kushindwa kutimiza hitaji hili ni upotevu wa rasilimali watu na nguvu ya kiuchumi. Stadi za vijana hazijawahi kuwa muhimu kiasi hiki.

Ripoti ya dunia ya ufuatiliaji inatukumbusha kwamba elimu sio tu kuhusu kuhakikisha kwamba watoto wanaenda shule. Bali ni kuhusu kuwaandaa vijana kwa maisha ya baadaye, kwa kuwapa fursa za kupata kazi bora, kupata kipato na kuchangia kwenye jumuiya na jamii zao na kutimiza ndoto zao. Na kwa mapana yake, ni kuhusu kuzisaidia nchi kukuza nguvu kazi zinazohitaji ili kuendelea kwenye uchumi wa dunia

Kumekuwa na maendeleo ya wazi kwenye malengo sita yaEFA – yakijumuisha kupanuka kwa elimu ya awali na kuongezeka kwa usawa wa kijinsia katika elimu ya msingi. Ingawa, miaka mitatu ikiwa imebaki kabla ya kufikia mwaka 2015 ambao ndio wa mwisho, dunia bado haiko kwenye hali nzuri. Maendeleo ya kufikia baadhi ya malengo hayatii moyo. Idadi ya watoto ambao hawaendi shule imesimama kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2000. Elimu ya watu wazima na ubora wa walimu bado vinahitaji maendeleo ya haraka

Hali ya sasa inaonyesha kwamba kuna haja kubwa ya kuhakikisha kunakuwa na usawa kwenye mipango ya kuendeleza stadi sahihi. Kwa kuwa idadi ya watu inaongezeka kwa maeneo ya mijini, hususani kwenye zinazoendelea, vijana wanahitaji stadi za kuwatoa kwenye umaskini, kwenye maeneo ya vijijini, vijana wanahitaji njia mpya za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kupungua kwa ukubwa wa mashamba na kutumia fursa za kazi nje ya kilimo. Ripoti hii inaonyesha kwamba takribani vijana milioni 200 wanahitaji nafasi nyingine ya upata stadi za kusoma na kuandika ambazo ni muhimu kwa ajili ya kujifunza stadi nyingine za kazi. Katika wote hawa, wanawake na maskini ndio wanaopata shida sana.

Lazima tuone kwamba idadi inayoongezeka ya vijana wasio na ajira au walionaswa kwenye umaskini kama jambo linalohitaji kuchukua hatua ya haraka – kutimiza mahitaji yao ifikapo mwaka 2015 na kuendelea na kasi hiyo hiyo baada ya hapo.
Tunaweza kufikia lengo la elimu ya sekondari kwa wote ifikapo mwaka 2030 na ni lazima

Dhamira ya wafadhili kusaidia elimu inaweza kuwa imepungua, na hii inatia wasiwasi sana. Bajeti za serikali zipo kwenye shinikizo siku hizi, lakini tusikubali kupoteza mafanikinio yaliyopatikana tangu mwaka 2000 kwa kupunguza juhudi sasa. Ushahidi kwenye Ripoti hii unaonyesha kwa pesa zinazotumika kwenye elimu zinazalisha mara kumi hadi kumi na tano zaidi kwenye ukuaji wa uchumi wa mtu katika maisha yake. Sasa ni wakati wa kuwekeza kwa maisha ya baadaye

Lazima tuwe wabunifu na kutumia rasilimali zote tulizo nazo. Serikali na wafadhili lazima waendelee kutoa kipaumbele kwenye elimu. Nchi inabidi zitegemee rasilimali zao zenyewe ambazo zinaweza kuwapa mamilioni ya watoto na vijana stadi kwa ajili ya maisha yao. Kwa kila chanzo cha fedha, mahitaji wa watu waliosahaulika lazima yapewe kipaumbele katika kila mkakati

Vijana popote wana uwezo mkubwa – huu lazima uendelezwe. Natumaini Ripoti hii itachochea juhudi mpya duniani za kuelemisha watoto na vijana ili waweze kuishi duniani



Irina Bokova
Mkurugenzi Mkuu, UNESCO

# Utangulizi

Wakati imebaki miaka mitatu kabla kufikia mwisho wa Malengo ya elimu kwa wote ambayo yaliwekwa Dakar, Senegal, ni suala la haraka kuhakikisha kwamba ahadi zilizowekwa na nchi 164 mwaka 2000 zinatekelezwa. Mambo yaliyojitokeza inabidi yatumiwe kwa ajili ya kuandaa malengo yajayo ya kimataifa kuhusu elimu na kuandaa njia za kuhakikisha kwamba wadau wote wanatimiza ahadi zao.

Kwa bahati mbaya, Ripoti ya mwaka huu ya ufuatiliaji wa EFA duniani inaonyesha kwamba kuna maendeleo kidogo kwenye kutimiza malengo mengi na kwamba malengo mengi ya EFA hayataweza kufikiwa. Pamoja na picha isiyo tia moyo, maendeleo kwenye baadhi ya nchi maskini yanaonyesha kile kinachoweza kufikiwa kwa juhudi za serikali na misaada ikijumuisha idadi kubwa ya watoto wanaoenda shule ya awali, wanaomaliza shule ya msingi na wanaondelea na elimu ya sekondari

Ripoti ya ufuatiliaji wa malengo ya EFA 2012 imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaonyesha kwa ufupi kiwango cha maendeleo kwenye malengo sita ya EFA na kutumia fedha kufikia malengo ya elimu. Sehemu ya pili inahusu lengo la tatu la EFA, likiweka mkazo mkubwa kwenye stadi zinazohitajika kwa vijana.

## Mambo Muhimu

- Lengo la 1: Uboreshaji wa elimu ya awali umekuwa ukienda taratibu mno. Mwaka 2010, takribani 28 % ya watoto chini ya miaka mitano walikuwa wamedumaa, na chini ya nusu ya watoto wote duniani walipata elimu ya awali

- Lengo la 2: Maendeleo kuelekea elimu ya msingi kwa wote bado ya yanasuasua. Idadi ya watoto wasioenda shule imesimama kwenye milioni 61 mwaka 2010. Kati ya watoto 100 wasioenda shule, 47 hawategemewi kujiunga na shule

- Lengo la 3: Vijana wengi wanakosa stadi za msingi. Kwenye nchi 123 zenye kipato cha chini na cha kati, takribani vijana milioni 200 wenye umri kati ya Miaka 15 na 24 hawajamaliza elimu ya msingi ambayo ni sawa na kijana mmoja kati ya watano

- Lengo la 4: Elimu ya watu wazima imebaki kuwa lengo la kufikirika. Idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika imeshuka kwa asilimia 12 kati ya mwaka 1990 na 2010. Mwaka 2010, takribani watu wazima milioni 775 walikuwa hawajui kusoma na kuandika, theluthi mbili kati ya watu hao walikuwa ni wanawake

- Lengo la 5: Tofauti za kijinsia zimechukua miundo tofauti.
  Mwaka 2010, bado kulikuwa na nchi kumi na saba ambapo kulikuwa na tofauti ya wasichana tisa kwa kila wavulana kumi kwenye shule ya msingi. Na katika zaidi ya nusu ya nchi tisini na tisa ambazo hazijafikia lengo la usawa wa kijinsia, wavulana wako kwenye hali ngumu


- Lengo la 6: Tofauti ya matokeo ya kujifunza duniani bado haijabadilika. Takribani watoto milioni 250 hawawezi kusoma au kuandika wanapofika darasa la 4








# Sehemu ya 1. Ufuatiliaji wa Malengo ya Elimu kwa wote



**Watoto milioni 171 walio chini ya miaka 5 walikuwa wameathiriwa na udumavu wa wastani au mkali mwaka 2010**

## Malengo sita ya elimu kwa wote

*Kupanua elimu ya awali*. Kipindi cha utoto ni muhimu sana kuweka misingi ya mafanikio kwenye elimu na siku za baadaye, hivyo elimu ya awali inapaswa kuwa msingi wa EFA na malengo makubwa ya maendeleo.

Watoto wenye njaa, utapiamlo au wanaoumwa hawana nafasi nzuri ya kupata stadi wanazozihitaji kwa ajili ya kujifunza na ajira kwa siku za baadaye. Kuna dalili kwamba afya za watoto zinaimarika, lakini kwa kasi ndogo katika baadhi ya nchi na sio kwa kasi ya kufikia malengo ya kimataifa ya maendeleo. Wastani wa mwaka kwa vifo vya watoto umeongezeka kutoka 1.9% kwaka 1990-2000 hadi 2.5% mwaka 2000-2010. Makadirio ya karibuni yanaonyesha kwamba zaidi ya nusu ya vifo vya watoto vinahusiana zaidi na elimu ya wanawake wakati wa umri wa uzazi

Inatia moyo kwamba leo zaidi ya watoto 3 kati ya watoto 100 wanaozaliwa wakiwa hai tofauti na mwaka 1990, bado kuna nchi 28, ambapo 25 kati ya hizo zipo Afrika kusini mwa jangwa la Sahara, ambapo zaidi ya watoto 10 kati ya 100 hufa kabla ya miaka 5

Sababu kubwa ya vifo hivi ni utapiamlo ambao hudumaza ukuaji wa ubongo na uwezo wa kujifunza. Kudumaa au kuwa mfupi kulinganisha na umri husika ni ishara ya wazi ya utapiamlo. Duniani watoto milioni 171 walio chini ya miaka 5 walikuwa wameathiriwa na udumavu wa wastani au mkali mwaka 2010. Ifikapo mwaka  2015, kulingana na hali ya sasa, idadi ya watoto wanaoathirika na udumavu itakuwa milioni 157 au takribani mtoto mmoja kati ya wanne walio chini ya miaka 5.

Watoto kwenye maeneo ya vijijini na kutoka kwenye familia maskini wanaathirika zaidi kwa sababu lishe sio tu suala la upatikanaji wa chakula. Bali  ni suala la kupata chakula, huduma  nzuri za afya, maji na, huduma  ya vyoo ambazo watu masikini wanazikosa Kwa mfano Nepal, kiwango cha udumavu kilikuwa 26% miongoni mwa watoto kutoka familia tajiri na 56% kutoka familia maskini, na kiwango 27% kwenye maeneo ya mijini na 42% kwenye maeneo ya vijijini. Hali inayoendelea ya kupanda na kushuka kwa bei ya chakula, mabadiliko ya tabia nchi na migogoro vinafanya uboreshaji wa lishe kuwa changamoto kwenye sehemu nyingi za dunia

Lakini uzoefu unaokinzana kwenye nchi nyingi unaonyesha kwa utashi wa kisiasa unaweza kwa kiasi kikubwa kuboresha lishe. Chini ya miongo miwili, Brazil imeweza kuondoa tofauti kati mijini na vijijini kwenye suala la utapiamlo kutokana na kuboresha elimu ya akina mama, kutoa huduma za mama na mtoto, usambazaji wa huduma ya za maji na vyoo na uhamishaji wa jamii lengwa. Kwenye kipindi hicho hicho, viwango vya utapiamlo hususani kwenye maeneo ya vijijini kwenye nchi kama Bolivia, Guatemala na Peru vilibaki kuwa juu kuliko matarajio ya kiwango cha kipato

Mipango bora ya elimu ya awali ni muhimu kwa ajili ya kuwaandaa watoto kwa ajili ya shule. Ushahidi kutoka sehemu mbalimbali kama Australia, India, Msumbiji, Uturuki na Uruguay unaonyesha faida za muda mfupi na mrefu za elimu ya awali. Hizi zinatofautiana kutoka kuanzia stadi za kusoma na kuhesabu hadi kuongezeka kwa umakini, juhudi na kuchukua hatua – zote hizi zinapelekea matokeo mazuri ya elimu na ajira

Ushahidi wa karibuni kutokana na utafiti wa mwaka 2009 kuhusu tathmini ya mpango wa wanafunzi wa kigeni kwenye nchi za OECD unaonyesha kwamba nchi hamasini na nane kati ya sitini na tano, wanafunzi wenye miaka 15 ambao walikaa mwaka mmoja kwenye shule ya awali walikuwa na uwezo mkubwa kuliko wale ambao hawajawahi kwenda shule ya awali hata baada kuzingatia historia ya kiuchumi na kijamii. Australia na Brazil na Ujerumani, wastani wa matokeo baada ya kuzingatia historia ya kiuchumi na kijamii ilikuwa sawa na mwaka mmoja wa masomo

Tangu mwaka 1999, idadi ya watoto wanaoandikishwa kwenye elimu ya awali imeongezeka kwa takribani nusu. Ingawa hii inafanya, mtoto mmoja kati ya wawili haendi shule, na kuongezeka hadi watano kati ya sita katika nchi maskini. Makundi ambayo yangefaidika zaidi na elimu ya awali bado yanaikosa. Nchini Nigeria, takribani watoto wawili kati ya watatu kutoka 20% ya familia tajiri wanaenda kwenye shule za awali, ukilinganisha na chini ya mtoto mmoja kati ya kumi kutoka 20% ya familia maskini

Uwekezaji mdogo ni sababu kubwa ya kutokuwa na idadi kubwa za shule za awali. Kiwango hiki ni chini ya 10% ya bajeti ya elimu kwenye nchi nyingi. Nepal na Niger zinatumia chini ya 0.1% ya pato la taifa kwa ajili ya elimu ya awali na Madagascar na Senegal chini ya 0.02%

Moja ya matokeo ya uwekezaji mdogo wa serikali ni wastani wa watoto wanaoandikishwa kwenye shule za awali za binafsi ambao ni 33%. Nchini Siria, yenye kiwango cha uandikishaji cha 10% kwenye shule za awali, 72% wapo kwenye shule za binafsi. Hii inaonyesha hitaji lisilo timizwa na sekta ya umma

Haonekani kama kuongeza idadi ya shule za awali za kulipia kutawafikia watoto kutoka familia maskini zaidi ambazo watoto wake wana uwezekano mdogo wa kuandikishwa.
Kwenye jimbo la Andhra Pradesh nchini India uandikishaji uko juu kwenye maeneo ya vijijini kutoka kwenye 20% ya familia tajiri ambapo takribani theluthi moja ya watoto
wanaenda kwenye shule binafsi. Takribani watoto wote kwenye shule za awali wanaotoka kwenye familia maskini wanahudumiwa na serikali

Mahali ambapo watoto wanaishi kunaweza kuonyesha ubora wa huduma. Kwenye maeneo ya vijijini ya China, Peru na Tanzania, watoto wanaoenda kwenye shule za awali wana uwezekano mkubwa kuliko wale kutoka maeneo ya mijini; kusoma kwenye madarasa yaliyojaa, yenye walimu wasio na ujuzi na yenye vifaa vichache vya kujifunzia


Ili kuhakikisha kwamba watoto wote wanafaidika na matunda ya elimu ya awali, mabadiliko yanahitajika, yakijumuisha ongezeko la vifaa na kuhakikisha vinapatikana kwa gharama nafuu, kugundua njia sahihi za kuunganisha elimu ya awali na ya msingi na kuratibu mazoezi ya elimu ya awali na mikakati inayohusu kipindi cha utoto
Umuhimu wa kuweka usawa kwenye juhudi za kuboresha mazingira kwa ajili ya watoto wadogo unaonyeshwa zaidi na farihisi mpya zilizoandaliwa kwa ajili ya Ripoti ya mwaka huu ambayo inatathmini maendeleo kwenye lengo hili na sehemu zake tatu: afya, lishe na elimu

Alama za baadhi ya nchi ni takribani sawa kwenye viashiria vitatu (kwa mfano Chile) au ni dhaifu

**Senegal inatumia chini ya 0.02% ya mapato ya taifa kwa elimu ya awali**

**Mchoro wa 1: Ushiriki katika elimu ya awali unatofautiana kulingana na nchi**

Kiwango cha mahudhurio katika elimu ya awali kwa watoto wenye umri kati ya miezi 36 na 59, kwa kuzingatia utajiri, mahali na jinsia




Zingatia: Umri rasmi wa kuanza elimu ya awali ni kuanzia miaka 3 hadi 5 katika nchi hizo tatu. Nchini Nigeria, kiwango cha 40% ya watu masikini kinaonyeshwa kwa aijili ya watu wanaoishi mijini.

Chanzo: Mahesabu (2012) ya timu iliyoandaa Ripoti ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote duniani kutokana na viashiria mbalimbali vya taarifa zilizoandaliwa na Kikundi cha Uchunguzi


(kwa mfano Niger). Nyingine zina alama za juu sana au za chini sana kwenye kipengele kimoja kulinganisha na alama za jumla kwenye farihisi, ambapo inaonyesha changamoto maalum. Kwa mfano, Jamaica na Philippines zote zina kiwango cha vifo vya watoto cha 30 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai lakini zina rekodi tofauti za elimu. 38% tu ya watoto wenye miaka 3 hadi 7 wameandikishwa kwenye elimu ya awali au elimu ya msingi nchini Philippines ukilinganisha na 90% nchi Jamaica. Hii inaonyesha hitaji la kuwekeza kwenye mikakati jumuishi ambayo inatoa umuhimu sawa kwenye usawa kwenye nyanja zote za ukuaji wa mtoto

Kulingana na hali ya sasa, lengo la elimu ya msingi kwa wote (UPE) halitaweza kufikiwa kwa kiwango kikubwa. Msukumo mkubwa wa kuhakikisha watoto watototoengi zaidi wanaenda shule ulioanzishwa kwenye Mkutano wa Dunia kuhusu Elimu huko Dakar mwaka 2000 bado unasuasua. Idadi ya watoto wenye umri wa kwenda ili hali hawaendi imepungua kutoka milioni 108 hadi milioni 61 kutoka mwaka 1999, ingawa robo tatu ya kupungua huko kumetokea kati ya 1999 na 2004. Kati ya 2008 na 2010 kwa ujumla hakukuwa na maendeleo (Kielelezo 2)

Kusini na Magharibi ya Asia na Afrika kusini mwa jangwa la Sahahra zilianza katika nafasi zinazofanana mwaka 1999 zikiwa na takribani watoto milioni 40 wasioenda shule, lakini zimepiga hatua kwa kiwango tofauti. Kati ya 1999 na 2008, idadi ya watoto wasioenda shule Kusini na Magharibi ya Asia ilishuka hadi milioni 29 wakati kupungua katika nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara kulikuwa kwa kiwango kidogo, milioni 11

Mchoro wa 2: Idadi ya watoto ambao hawasomi ilipungua miaka ya mwanzoni baada ya Dakar, lakini kilichofuata ni kutuama, ina maana idadi haikuongezeka wala kupungua

Idadi ya watoto waliofikisha umri wa kuanza elimu ya msingi ambao hawasomi, 1999 – 2010




Vyanzo : Kiambatishi cha jedwali la 5 la Takwimu, Ghala – takwimu la UIS

Kati ya 2008 na 2010, idadi ya watoto wasioenda shule iliongezeka kusini mwa jangwa la Sahara kwa milioni 1.6, lakini ilipungua kwa laki 6 Kusini na Magharibi mwa Asia. Afrika kusini mwa Sahara sasa ina nusu ya watoto wote duniani wasiokwenda shule
Miongoni mwa nchi zenye takwimu, kumi na mbili zina takribani nusu ya watoto wote wasioenda shule duniani. Nigeria inaongoza orodha ambapo ina mtoto mmoja kati ya sita wasienda shule duniani, jumla ya watoto milioni 10.5 (kielelezo 3). Ilikuwa na watoto milioni 3.6 zaidi ya wale waliokuwa hawaendi shule 2010 kulinganisha na 2000. Katika hali tofauti, Ethiopia na India zimeweza kupunguza idadi ya watoto wasioenda shule kwa kiasi kikubwa. Nchini India, kulikuwa na watoto milioni 18 wachache zaidi waliokuwa hawaendi shule mwaka 2008 kulinganisha na 2001

Miongoni mwa wale wasioenda shule, baadhi wanaweza kujiunga baadaye, wakati wengine wanaweza kuacha shule na wasijiunge tena. Mwaka 2010, 47% ya watoto wasioenda shule walikuwa hawana uwezekano wa kujiunga tena. Kiwango kilikuwa cha juu katika nchi maskini, ambapo 57% ya watoto wasioenda shule wasingeweza kujiunga tena. Wasichana walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa katika kundi hili kulinganisha na wavulana.

Ikiwa imebaki miaka mitano kufika mwaka 2015, nchi ishirini na tisa zilikuwa na wastani wa uandikishaji wa chini ya 85%. Nchi hizi zina uwezekano mdogo wa kufikia lengo la UPE.


Watoto wenye umri rasmi wa kuanza shule ambao walikuwa hawaendi shule mwaka 2010 hawataweza kumaliza elimu ya msingi ifikapo mwaka 2015. Mwaka 2010, kulikuwa na nchi sabini zilizokuwa na kiwango cha uandikishaji cha chini ya 80%.

Changamoto ya UPE ni kuwapeleka watoto shule katika umri mwafaka na kuhakikisha kwamba wanaendelea na masomo na kuyamaliza. Uchanganuzi wa Ripoti hii unaonyesha kwamba, kati ya nchi ishirini na mbili zenye takwimu za utafiti kati ya 2005 na 2010, 38% ya watoto waliojiunga na shule walikuwa na miaka miwili au zaidi ya umri rasmi. Kwenye nchi za Afrika Kusini mwa Sahara zilizojumuishwa kwenye uchanganuzi, 41% za watoto wanaoanza elimu ya msingi walikuwa na miaka miwili au zaidi ya umri rasmi wa kuanza shule.

Watoto wengi kutoka familia maskini wanaanza masomo kwa kuchelewa, mara nyingi kwa sababu wanaishi mbali na shule, hali zao za kiafya na lishe ni mbaya au wazazi wao wanaweza kuwa na upeo mdogo kuhusu umuhimu wa kupeleka watoto shule kwa wakati. Nchini Colombia, 42% ya watoto kutoka familia maskini walianza shule na miaka miwili au zaidi ya umri rasmi, ukilinganisha na 11% kutoka familia tajiri.

Mchoro 3 : nchini Nigeria, idadi ya watoto ambao hawasomi na kubwa ni imeongezeka

Kiwango na idadi vya watoto waliofikisha umri wa kwenda shule ambao hawasomi, 2001 hadi 2010




Zingatia : ukubwa wa viduara unalingana na idadi ya watoto ambao hawasomi. Namba ndani ya viduara zinaonyesha idadi ya watoto ambao hawasomi. Tarakimu za Nigeria za mwaka 2001 ni za tangu mwaka 2000. Tarakimu za India ni za tangu mwaka 2008.
Chanzo: Ghala-takwimu la UIS

Kuchelewa kuanza kunaathiri uwezekano wa watoto wa kumaliza shule. Wakifika darasa la 3, watoto waliochelewa kuanza shule wanaweza kuwa na uwezekano mkubwa mara nne wa kuacha shule kulinganisha na wale walioanza katika umri sahihi.

Umaskini nao unaathiri uwezekano wa watoto kuacha shule mapema. Nchi Uganda, watoto 97 kati ya 100 kutoka asilimia ishirini ya familia tajiri walianza elimu ya msingi na 80 walimaliza masomo mwaka 2006; watoto 90 kati ya 100 kutoka kwenye asilimia ishirini ya familia maskini walianza shule lakini ni 49 tu ndio waliomaliza masomo.

Ili kukabiliana na vikwazo vinavyowazuia watoto kutoka familia maskini kuanza shule kwa wakati na kuendelea hadi mwisho, mabadiliko makubwa ya kimuundo yanahitajika. Katika nchi nyingi, gharama ni sababu ya msingi inayowafanya wazazi wasiandikishe watoto wao shule au kuwatoa shuleni. Hata baada ya kuwa ada za shule zimeondolewa rasmi, michango rasmi au isiyo rasmi ilichukua 15% ya gharama katika nchi nane zilizofanyiwa uchanganuzi katika Ripoti hii.

Familia tajiri zina uwezo wa kutumia kiasi kikubwa zaidi kwenye elimu ya watoto zao, kuongeza fursa zao za kupata elimu bora. Hii inajumuisha matumizi zaidi kwenye shule binafsi au masomo ya ziada. Nchini Nigeria, 20% ya familia tajiri hutumia mara kumi zaidi ya 20% ya familia maskini kugharamia elimu ya watoto. Hata ada zinapokuwa nafuu katika shule za binafsi, bado familia maskini haziwezi kumudu. Kupeleka watoto watatu shule kwenye maeneo ya watu maskini ya Lagos hugharimu 46% ya kiwango cha chini cha mshahara. , na uwezekano mkubwa wa kuwekeza kwanza katika masomo ya ziada.

Kuondoa ada rasmi za shule imekuwa hatua muhimu kufikia malengo ya UPE. Lakini ni muhimu pia kwa serikali kuchukua hatua nyingine sambamba na hiyo, kama kutoa ruzuku kwa shule ili kuzisaidia kumudu gharama zao ili wasitoze michango isiyo rasmi kwa wazazi. Mipango ya hifadhi ya jamii, kama uhamishaji wa fedha, ni muhimu ili kuhakikisha familia maskini zina uwezo wa kifedha kumudu gharama za shule bila kuathiri matumizi yao kwenye mahitaji ya msingi. Hatua pia inabidi zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa uwezo wa familia tajiri kugharamia masomo katika shule binafsi na masomo ya ziada hauongezi hali ya kutokuwa na usawa.

**Nchini Bangladeshi na Misri, familia tajiri hutumia mara nne zaidi ya familia maskini kugharamia masomo ya ziada**

### *Kuhamasisha kujifunza na stadi za maisha kwa vijana na watu wazima*

Changamoto za kijamii na kiuchumi za miaka ya karibuni zimejikita kwenye upatikanaji wa fursa za stadi na kujifunza kwa vijana. Kama kipengele kwenye Ripoti hii kinavyoonyesha, changamoto hizi zinaonyesha hali ya uharaka kuhusu umuhimu wa lengo ambalo halijapewa umuhimu unaostahili kwa sababu ya utata wa ahadi zilizotolewa wakati malengo ya EFA yanawekwa mwaka 2000.

Elimu rasmi ya sekondari ni njia nzuri ya kuendeleza stadi zinazohitajika kwa ajili ya kufanya na maisha. Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaojiunga na elimu ya sekondari duniani, uwiano wa kuandikisha katika elimu ya sekondari ya awali ulikuwa 52% katika nchi maskini mwaka 2010, ikiacha mamilioni ya vijana kukabiliana na maisha bila kuwa na stadi za msingi wanazohitaji ili kuishi maisha bora. Mwaka 2010, kulikuwa na vijana milioni 71 duniani wenye umri wa kwenda sekondari ya awali lakini walikuwa hawaendi. Idadi imebaki hiyo hiyo tangu mwaka 2007. vijana watatu kati ya wanne wasioenda shule wanaishi Kusini na Magharibi ya Asia na Afrika Kusini mwa Sahara.



Leo kuna 25% ya watoto walio kwenye shule za sekondari kuliko mwaka 1999. Afrika kusini mwa Sahara imeongeza mara mbili idadi ya wanafunzi wanaojiunga na sekondari katika kipindi hicho, ingawa ina kiwango cha chini zaidi ya uwiano wa kuandikisha elimu ya sekondari, 40% mwaka 2010.

Baadhi ya vijana wanakuza stadi kupitia elimu ya ufundi stadi. Kiwango cha watoto wanaoandikishwa kwenye elimu ya sekondari imebaki 11% tangu mwaka 1999.

Stadi hazikuzwi shuleni tu. Mashirika ya kimataifa yana mifumo tofauti ya kuainisha stadi na mipando ya kukuza stadi. Lakini miaka kumi na mbili tangu kuzinduliwa kwa malengo ya EFA huko Dakar, jumuiya ya kimataifa bado haijafikia mwafaka kabisa wa nini kinajumuisha maendeleo kwenye 'usawa katika kujifunza na mipango stahiki ya stadi za maisha' (msingi wa lengo la 3), kukubaliana kwenye vigezo mwafaka vya kimataifa kwa ajili ya kulinganisha na kufanya tathmini kama kuna maendeleo yaliyofikiwa. Kuna viashiria vya kutia matumaini kuwa hali inaweza kubadilika, lakini maendeleo ya karibuni hayatatoa takwimu za kutosha kwa wakati ili kupima kwa undani lengo la 3 kabla tarehe ya mwisho haijafika.

Malengo yoyote ya kimataifa baada ya mwaka 2015 yanahitaji kufafanuliwa kwa usahihi na kupanga vizuri jinsi ya kupima ya kupima maendeleo. Hii inabidi ijikite kwenye tathmini halisi ya taarifa ambazo zinaweza kukusanywa, ili kuepuka matatizo ambayo yalikwamisha juhudi za kufuatilia lengo la 3.

Azimio la Dakar linataja baadhi ya hatari ambazo kwazo vijana wanahitaji kulindwa kwa kukuza stadi sahihi za maisha. Moja ya hatari hizi ilikuwa VVU na Ukimwi. Elimu kuhusiana na Ukimwi bado iko chini. Makadirio ya karibuni kwenye nchi 119 duniani yanaonyesha kwamba 24% tu ya vijana wa kike na 36% ya vijana wa kiume walio na umri kati ya miaka 15 na 24 wanaweza kutambua njia za kujikinga na maambukizi ya VVU kupitia ngono na kuachana na dhana potofu kuhusu maambukizi yake.

Elimu ya Ukimwi na VVU ni ndogo hata kwenye nchi zenye viwango vya juu vya maambukizi. Mwaka 2007, takribani watoto 60,000 wa darasa la 6 (wenye wastani wa miaka 13) kwenye nchi 15 za kusini na mashariki mwa Afrika walifanyiwa tathimini ya ufahamu wao kuhusu VVU na Ukimwi. Tathmini iliyojikita kwenye mitaala rasmi ya elimu ya VVU iliyopitishwa na wizara za elimu katika nchi shiriki. Matokeo yanaonyesha utekelezaji mbovu na labda uandaaji duni wa mtaala. Kwa wastani, 36% tu ya wanafunzi walifikia kiwango cha chini cha ufahamu kinachohitajika na 7% tu walifikia kiwango kinachohitajika.

Haitoshi kuhakikisha kwamba vijana wanajua jinsi ya kulinda afya zao na afya za wengine, kama kwa mfano, hawajihisi kuwezeshwa kuchukua uamuzi sahihi kwa wakati sahihi.

Elimu ya stadi za maisha inayotilia mkazo VVU na Ukimwi inahamasisha vijana kujenga tabia ya kulinda afya zao, kwa mfano, kwa kuwawezesha kujadiliana kwenye mahusiano ya kingono. Inafanya hivyo kwa kuweka mkazo kwenye stadi za saikolojia ya jamii na mahusiano kama mawasiliano thabiti, kujiamini na kujadiliana. Mipango ya stadi za maisha ambayo inaweka mkazo kwenye mambo ya msingi katika namna ambayo inawawezesha wanafunzi kushiriki inabidi iingizwe ili kuongezea kwenye mada kwenye mtaala kama elimu ya afya na elimu pana ya VVU na Ukimwi.

*Kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika kwa 50%*

Kujua kusoma na kuandika ni kitu muhimu kwa ustawi wa kijamii na kiuchumi wa watu wazima na watoto wao. Ingawa maendeleo kwenye lengo hili yamekuwa madogo sana, kwa kiasi kikubwa ni matokeo ya kutojali kwa serikali na wafadhili. Mwaka 2010 bado kulikuwa na watu wazima milioni 775 wasiojua kusoma na kuandika. Nusu walikuwa kusini na magharibi ya Asia, na zaidi ya asilimia ishirini walikuwa Afrika kusini mwa Sahara.

Nchi 81 kati ya 146 zenye takwimu kwa mwaka 2005-2010, kulikuwa na wanawake wengi wasiojua kusoma kuliko wanaume. Kati ya nchi hizi, ishirini na moja zinaonyesha kutokuwa na usawa kwa kiwango cha juu, kukiwa na kwa uchache wanawake saba wasiojua kusoma na kuandika katika kila wanaume kumi.

Kiwango cha watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kimeongezeka katika miongo miwili iliyopita, kutoka 76% mwaka 1985-1994 hadi 84% mwaka 2005-2010. Lakini miongoni mwa nchi arubaini na tatu zenye kiwango cha chini ya 90% ya watu wazima wanaojua kusoma na kuandika kati ya mwaka 1998-2001, nchi tatu tu zitafikia lengo la kupunguza ujinga kwa 50% ifikapo mwaka 2015. Baadhi ya nchi hazitafikia lengo kwa kiwango kikubwa (Kielelezo 4).

Na wakati baadhi ya nchi kwenye kundi hilo zimepiga hatua kubwa – kwa mfano Mali, ambayo imeongeza mara mbili kiwango chake cha kujua kusoma na kuandika – nyingine kama Madagascar, zimeshuhudia kushuka kwa kiwango kwenye muongo uliopita.

Takribani robo tatu ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika wanaishi kwenye nchi kumi. 37% ya jumla yao duniani wanaishi India. Nchini Nigeria idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika imeongezeka kwa watu milioni 10 kwenye miongo miwili iliyopita na kufikia milioni 35.


Swali la msingi ni kama takwimu hizi zinaonyesha ukubwa wa tatizo. Watu wazima wanaulizwa kama wanajua kusoma na kuandika badala ya uwezo wao kujaribiwa. Njia za moja kwa moja za kupima stadi za watu wazima zinatoa picha nzuri ya stadi za kujua kusoma na kuandika.

Kwa kawaida inakisiwa kwamba inachukua miaka minne au mitano ya shule kwa watoto kuweza kusoma, kuandika na kufanya hesabu kwa urahisi. Hata hivyo, changanuzi mpya wa tafiti za familia kwa ajili ya Ripoti hii, unaonyesha,

**Robo tatu ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika wanaishi kwenye nchi kumi.**

Mchoro 4: nchi nyingi hazitofikia lengo la uwezo wa kusoma na kuandika kwa watu wazima, baadhi kwa kiwango kikubwa.

Kiwango cha kutojua kusoma na kuandika, 1998-2001 hadi 2015 (taswira)




Zingatia: nchi zilizoonyeshwa kwenye mchoro ni zile ambazo taswira ya mwaka 2015 iliwezekana na zilikuwa na kiwango cha kutojua kusoma na kuandika kwa watu wazima zaidi ya 10% miaka ya 1998 -2001Note:
Vyanzo: kiambatishi, jedwali la 2 la takwimu ; ghala-takwimu la UIS

Idadi kubwa zaidi ya watoto katika nchi maskini na zile za kipato cha kati wanamaliza elimu ya msingi bila kujua kusoma na kuandika kuliko inavyotegemewa. Nchini Ghana, kwa mfano, zaidi ya nusu ya wanawake na zaidi ya theluthi ya wanaume wenye umri kati ya miaka 15 na 29 ambao walimaliza darasa la sita ya shule walikuwa hawawezi kabisa kusoma sentensi mwaka 2008. 28% ya vijana wa kike na 33% ya vijana wa kiume walikuwa wanaweza kusoma sehemu ya sentensi (Kielelezo 5).

Mazingira ambamo watu wanaishi yanaweza kuathiri uwezo wao wa kujifunza na kuendeleza stadi zao za kusoma na kuandika. Matokeo ya awali ya Tathmini ya kujua kusoma na kuandika na Mpango wa ufuatiliaji huko Jordan, Mongolia, Palestine na Paraguay yanaonyesha kwamba viwango vya kujua kusoma na kuandika vinaweza kuficha tofauti kubwa katika mambo mengi na katika mazingira ambayo yanajenga stadi za kujua kusoma na kuandika kwa watu wazima.

**Nchi sitini na nane bado hazijafikia usawa wa kijinsia katika elimu ya msingi**

Kwenye nchi tajiri, elimu kwa wote imepelekea viwango vya juu vya kutojua kusoma na kuandika kuwa jambo la kihistoria / lililopitwa na wakati. Ingawa tathmini za moja kwa moja zinaonyesha kwamba mtu mzima mmoja kati ya watano katika nchi hizi, sawa na watu wazima milioni 160, wana stadi duni za kujua kusoma na kuandika- hawawezi kutumia stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa usahihi katika maisha yao ya kila siku, kwa mfano kuomba kazi au kuelewa maelezo kwenye chupa ya dawa. Wale wanaoishi kwenye mazingira duni ya kijamii, kama maskini, wahamiaji na makabila yenye watu wachache, ndio waathirika wakubwa.

Watu wenye stadi duni za kusoma na kuandika mara nyingi wananyanyapaliwa na mara nyingi hawajiamini. Hii ni changamoto kubwa kwa mikakati ya elimu ya watu wazima. Mipango ambayo inawasaidia washiriki kufaidika na matumizi ya stadi za kusoma na kuandika katika maisha yao ya kila huwatia moyo kushiriki huku wakiepuka unyanyapaa unaotokana na ushiriki wao.

Kiwango cha juu cha utashi wa kisiasa, na dira ya muda mrefu na ya kisera inayoenda sambamba na vifaa vya kutosha, inahitajika kupambana na tatizo hili.

### *Kufikia usawa wa kijinsia*

Usawa wa kijinsi katika elimu ni ya haki ya msingi ya binadamu, na pia njia muhimu ya kuboresha matokeo mengine ya kijamii na kiuchumi. Kupunguza tofauti ya kijinsia kwenye uandikishaji wa elimu ya msingi ni moja ya mafanikio makubwa ya EFA tangu mwaka 2000. Hata hivyo nchi nyingi bado zina uwezekano mdogo wa kufikia usawa wa kijinsia kwenye elimu ya msingi na sekondari ifikapo mwaka 2015. Na mambo mengi inabidi yafanywe ili kuhakikisha kwamba fursa za elimu na matokeo yanapatikana kwa usawa.


Nchi sitini na nane bado hazijafikia usawa wa kijinsia katika elimu ya msingi, na wasichana ndio waathirika zaidi katika nchi sitini miongoni mwao. Wakati nchi kama Ethiopia na Senegal zimepiga hatua kubwa, nyingine kama Angola na Eritrea zimerudi nyuma.

Idadi ya nchi ambazo wasichana wameathirika zaidi, au fahirisi ya usawa wa kijinsia iko chini ya 0.70, imeshuka kutoka kumi na sita mwaka 1990 hadi kumi na moja mwaka 2000, na hadi moja tu mwaka 2010- Afghanistan (Kielelezo 6). Pamoja na nafasi yake mwisho kwenye orodha, Afghanistan imepiga hatua kubwa katika miaka ya karibuni.

Hali mbaya zaidi – inayopimwa kwa fahirisi ya usawa wa kijinsi iliyo chini ya 0.90 – iko chini kuliko miaka kumi iliyopita. Kati ya nchi 167 zenye takwimu kati ya mwaka 1999 na 2010, thelathini na tatu zilikuwa na fahirisi ya usawa wa kijinsia chini ya 0.90 mwaka 1999, ikijumuisha nchi ishirini na moja za Afrika kusini mwa Sahara.

**Mchoro 5: Kwa vijana wengi, miaka sita shuleni haitoshi kujenga uwezo wa kusoma na kuandika**

Hali ya kujua kusoma na kuandika, wanaume na wanawake wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 29 waliomaliza darasa la sita, nchi zilizoteuliwa tangu 2005 hadi 2011 (%)




Chanzo: utafiti wa timu iliyoandaa Ripoti ya Ufuatiliaji wa Elimu kwa Wote Duniani (2012) kutokana na taarifa za uchunguzi wa kidemografia na kiafia

Hadi mwaka 2010, kulikuwa na nchi kumi na saba tu kwenye kundi hili, zikiwamo kumi na mbili za Afrika kusini mwa Sahara. Nchi ambazo zimepiga hatua kubwa kufikia usawa wa kijinsia, kama Burundi, India na Uganda, zinaonyesha nini kinaweza kufanywa wakati mikakati inapowekwa kuongeza ushiriki wa wasichana katika elimu, kama vile, kuhamasisha jamii, kuweka lengo la msaada wa kifedha kwa wasichana, kuhakikisha njia na vifaa vya kufundishia vyenye kujali usawa wa kijinsia vinatumika, kuweka mazingira ya shule salama na yenye afya.


Kuelewa sababu za uandikishaji mdogo wa wasichana ni muhimu ili kufikia lengo la usawa wa kijinsia.

Uchanganuzi wa takwimu za utafiti wa familia kwa ajili ya Ripoti kwenye nchi tisa unaonyesha kwamba wasichana wanakabiliana na vikwazo vingi vya kuanza elimu ya msingi kuliko wavulana, lakini wanapokuwa shuleni wana nafasi sawa ya kumaliza shule. Nchini Guinea kwa mfano, wasichana 40 kati ya 100 kutoka kwenye familia maskini humaliza elimu ya msingi, ukilinganisha na wavulana 52. Hii ni kwa sababu wasichana wachache huanza shule : wasichana 44 kati ya 100 kutoka familia maskini huanza shule, ukilinganisha na wavulana 57.

Katika zaidi ya nusu ya nchi tisini na saba zenye usawa wa kijinsia katika elimu ya sekondari, kuna wavulana wachache kuliko na wasichana.

Mchoro 6: Kumekuwa na maendeleo katika kupunguza tofauti ya kijinsia lakini wasichana bado wanakabiliana na vizingiti ili kupata fursa ya kusoma

Ishara ya usawa wa kijinsia katika kiwango cha uandikishaji wa jumla, nchi zenye Ishara ya Usawa wa kijinsia chini ya 0.90 mwaka 1990, kuanzia mwaka 1990 hadi 2000 na kuanzia mwaka 2000 hadi 2010




Zingatia: nchi pekee zenye taarifa za mwaka 1990,2000 na 2010 ndizo zilizoonyeshwa. Kama hakuna taarifa za mwaka Fulani, ina maana taarifa hizo ziliandaliwa kwa ajili ya kabla na baada ya miaka miwili.
Nchi za Afganistan na Oman hazikuwekwa kwa sababu zilikabiliana na mwelekeo hasi
Chanzo: ghala-takwimu la UIS

Nchi hizi ni tajiri na zina kiwango cha juu cha uandikishaji. Nyingi kati ya hizo zipo Amerika ya Kusini na Caribbean na Mashariki ya Asia na Pasifiki. Lakini pia kuna nchi tatu maskini ambapo wavulana ni waathirika : Bangladeshi, Myanmar na Rwanda.

Sababu kubwa inayowafanya wavulana waache shule ni umaskini na kuvutwa na soko la ajira, kama inavyoonekana Amerika Kusini na Caribbean. Kwa mfano, nchini Honduras wavulana sita kati ya kumi wenye umri kati ya miaka 15 na 17 walikuwa wanafanya kazi ya mshahara, kati yao ni wawili tu waliokuwa wanasoma. Kinyume chake, wasichana wawili kati ya kumi walikuwa wanafanya kazi ya mshahara.

Wavulana wanaweza kuacha shule kutokana na mazingira ya shule, ikiwemo mtazamo wa walimu. Ingawa tofauti ya mbinu za kujifunza kati ya wavulana na wasichana zina tofauti ndogo zaidi ya kufanana, walimu inabidi wajue tofauti hizo pale zinapokuwepo, na wawe tayari kubadilisha njia zao za kufundishia na kufanya tathmini. Njia mbili ambazo zimejaribiwa lakini zimeonyesha kukosa ufanisi katika baadhi ya mazingira ni shule za jinsi moja na kugawa madarasa kulingana na ufaulu.

**Katika zaidi ya nusu ya nchi tisini na saba zenye usawa wa kijinsia katika elimu ya sekondari, kuna wavulana wachache kuliko na wasichana.**

Wavulana pia wanakumbana na ugumu kwenye matokeo ya kujifunza, hususani kusoma. Kwa muda mrefu, pengo la kijinsia limekuwa likikua likiwaathiri zaidi wasichana. Wavulana wanaendelea kupata ugumu kwenye hisabati, lakini kuna ushahidi kwamba pengo hili linaweza kupungua.

Hakuna tofauti kubwa kwenye uwezo wa wasichana au wavulana kufanya vizuri kwa kiwango sawa wakiwa shuleni. Ili kupunguza pengo kwenye kusoma, wazazi, walimu na watunga sera inabidi wabuni mbinu za kuwachochea wavulana kusoma zaidi, ikihusisha kutumia shauku yao ya kutumia nakala za kidigitali. Ili kupunguza pengo la hisabati, maendeleo kwenye usawa wa kijinsia nje ya shule, hususani kwenye fursa za ajira, yanaweza kutoa mchango mkubwa kupunguza tofauti.


### *Kuongeza ubora wa elimu*

Miongoni mwa watoto milioni 650 duniani wenye umri wa kwenda shule, ni wakati mwafaka wa kuweka mkazo sio tu kupunguza hadi milioni 120 wale wasiofika darasa la 4 bali pia ongezeko la milioni 130 wale ambao wanasoma lakini wanashindwa kujifunza stadi za msingi.

Uchanganuzi wa miundo ya kukosa usawa kwenye matokeo ya kujifunza na sababu zake, unaweza kusaidia kuboresha sera ambazo zitawasaidia watoto kutoka familia maskini kuvishinda vikwazo. Katika nchi sabini na nne ambazo zilishiriki kwenye utafiti wa PISA mwaka 2009, kadri mtoto anavyokuwa kwenye asilimia ya familia ishirini zenye fahirisi ya juu ya kijamii na kiuchumi, ndivyo anavyokuwa na matokeo mazuri, hali ikiwa hivyo hivyo kwa wavulana na wasichana (Kielelezo 7).

Mchoro wa 7: Mafanikio ya elimu yanatofautiana kulingana na hali ya kijamii na kiuchumi

Mchoro wa 7: Mafanikio ya elimu yanatofautiana kulingana na hali ya kijamii na kiuchumi
Asilimia ya wanafunzi kwenye au juu ya ngazi ya 2 katika hisabati kulingana na hali ya kiuchumi,kijamii, kitamaduni na kijinsia, PISA 2009




Zingatia: nchi zilizoshiriki kwenye PISA 2009, Azerbaijan, Himachal Pradesh (India) na Liechtenstein hazikumuishwa. Maneno Masikini/tajiri yanawakilisha sehemu ya chini/juu ya mchoro katika ishara ya hali PISA kiuchumi, kijamii na kitamaduni

Chanzo: Altinok (2012b), kulingana na taarifa za PISA 2009: Walker (2011)

Kwenye nchi za kipato cha kati zilizoshiriki kwenye tathmini, matokeo ya mwanafunzi yalikuwa chini sana : kwa wastani, zaidi ya nusu walipata alama chini ya 2 kwenye hisabati. Hata hivyo, baada ya kipindi fulani, baadhi ya nchi zenye kipato cha kati zimeweza kuongeza wastani wa alama na kupunguza hali ya kutokuwa na usawa kwenye matokeo ya kujifunza. Asilimia ya wenye matokeo ya chini katika kila asilimia ishirini ya kiwango fulani cha hali ya kijamii na kiuchumi nchini Brazil na Mexico kilishuka kati ya 2003 na 2009. Hii inatia moyo kwa sababu ushiriki kwenye elimu ya sekondari uliongezeka sana kwenye kipindi hicho. Sera za hifadhi ya jamii zenye malengo fulani ambazo zimekuwa zikitekelezwa kwenye nchi hizi tangu miaka ya mwisho ya 1990 ni sababu ya mafanikio yaliyopatikana miongoni mwa wanafunzi kutoka familia maskini.

Walimu ni sehemu muhimu sana ya uboreshaji kujifunza. Katika maeneo mengi, upungufu wa walimu, hususani walimu waliopata mafunzo, imekuwa kikwazo kikubwa cha kufikia malengo ya EFA. Makadirio ya karibu yanaonyesha kwamba nchi 112 zinahitaji kuongeza jumla ya idadi ya walimu wa shule za msingi milioni 5.4 ifikapo mwaka 2015. Walimu wapya wanahitajika ili kujaza nafasi za ziada milioni 2 zinazohitajika ili kufikia lengo la elimu ya msingi kwa wote na nafasi milioni 3.4 za wale wanaoachana na fani hiyo. Nchi za Afrika kusini mwa Sahara pekee zinahitaji kuajiri zaidi ya walimu milioni 2 il kufikia lengo la UPE.

Uwiano wa idadi ya walimu wa shule ya msingi na wanafunzi ni moja ya vipimo vya ubora wa elimu. Uwiano wa mwanafunzi / mwalimu duniani ulipungua kutoka 26 :1 mwaka 1999 hadi 24 :1 mwaka 2010. Afrika kusini mwa Sahara, pamoja na kuajiri zaidi ya walimu milioni 1.1, uwiano wa mwanafunzi/mwalimu uliongezeka kidogo, kutoka 42 :1 hadi 43 : 1, kutokana na kuongezeka kwa kasi kwa kiwango cha uandikishaji.

Kati ya nchi 100 zenye takwimu za elimu ya msingi, katika nchi thelathini na tatu chini ya 75% ya walimu walipata mafunzo kwa viwango vya kitaifa. Walimu inabidi wapewe mafunzo stahiki ili kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Tathmini zimeonyesha kwamba watoto kwenye nchi nyingi wanaweza kutumia miaka mingi shuleni bila kujifunza kusoma neno lolote. Nchini Mali, kwa mfano, zaidi ya watoto wanane kati ya kumi wa darasa la 2 hawakuweza kusoma hata neno moja katika lugha ya taifa. Ni matokeo ya kushangaza kiasi cha kuangalia upya jinsi walimu wanavyofundishwa, na msaada wanaopata mara wanapoingia darasani.

Walimu wenyewe wanaweza wasiwe na ufahamu wa kutosha wa somo husika wanapojiunga na vyuo vya ualimu, hivyo kozi zinaweka mkazo wa kukuza ufahamu wa msingi wa somo kuliko kujifunza jinsi ya kufundisha kwa ufanisi.
Mbali na hilo, maendeleo ya kitaaluma husimama mara tu walimu wanapoingia darasani.

Serikali zinabidi kuchukua hatua thabiti kuimarisha ufundishaji kwenye hatua zote. Mafunzo ya awali inabidi yaongeze mkazo kwenye njia za kufundisha darasani zenye ufanisi. Mafunzo kazini yanaweza kuwashirikisha walimu ili kuhakikisha kuwa maarifa yanabadilishwa kuwa vitendo vyenye ufanisi darasani. Faida zinaweza kuonekana zaidi mafunzo yanapohusishwa na njia nyingine, kama uboreshaji wa vifaa vya ufundishaji.

### *Farihisi ya maendeleo ya elimu kwa wote*

Farihisi ya maendeleo ya elimu kwa wote (EDI) inatoa picha ya haraka ya maendeleo ya jumla ya mifumo ya elimu ya taifa ili kufikia lengo la Elimu kwa wote. Katika kikundi cha nchi hamsini na mbili, inawezekana kufuatilia mabadiliko ya Farihisi ya maendeleo ya elimu kwa wote (EDI) tangu Mkutano wa Dunia wa Elimu huko Dakar. Farihisi ya maendeleo ya elimu kwa wote (EDI) imeboreka katika nchi arubaini na moja kati ya hamsini na mbili kati ya mwaka 1999 na 2010. Ongezeko kubwa lilitokea katika nchi kumi na mbili za Afrika kusini mwa Sahara zilizo katika kundi hili, ambapo Ethiopia na Msumbiji zimekuwa na ongezeko la haraka sana.

**nchi 112 zinahitaji kuongeza jumla ya idadi ya walimu wa shule za msingi milioni 5.4 ifikapo mwaka 2015.**

Matokeo kama haya yanaweza kuficha tofauti kwenye juhudi ambazo nchi inafanya ili kufikia malengo ya EFA. Kwa mfano, Colombia na Tunisia zina alama sawa za Farihisi ya maendeleo ya elimu kwa wote (EDI). Tunisia ina viwango vya juu cha uandikishaji na kubaki shuleni lakini ina kiwango cha chini cha kujua kusoma na kuandika miongoni mwa watu wazima. Colombia ina kiwango cha juu cha kujua kusoma na kuandika miongoni mwa watu wazima lakini ina viwango vya chini vya uandikishaji na kubaki shuleni. Kiwango cha chini cha elimu ya wazima nchini Tunisia kinaonyesha sehemu ya historia yake na sio lazima iwe juhudi zake za sasa wakati alama za chini za Colombia kwenye viashiria vinavyohusiana na watoto walio katika umri wa elimu ya msingi zinaonyesha kwamba inaweza kuwa na kiwango cha chini cha elimu ya watu wazima katika miaka ya baadaye.

Kupanua EDI ili kujumuisha Farihisi ya ECCE iliyoandaliwa kwa ajili ya Ripoti hii inaonyesha kwamba nchi hizi zimeweka mkazo mkubwa kwenye elimu ya awali. Baadhi ya nchi – hususani huko Asia ya Kati, kama Kyrgyzstan na Mashariki ya Asia kama Indonesia na Philippines – zimeshuka katika viwango, wakati nchi kama Jamaica na Mexico zimeboresha viwango vyao.

EFA haiwezi kufikiwa kama mkazo hautawekwa kwenye malengo yote. Hii inahitaji mkazo maalum kwenye yale yaliyosahaulika, ikiwemo ECCE na elimu ya watu wazima. Kuvunja mzunguko wa kukosa elimu kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kutoa elimu bora kwa watoto wote, ikijumuisha katika miaka yao ya mwanzo ya maisha, na wazazi wao, ni muhimu.

# Ukosefu wa usawa duniani

Pamoja na uchapishaji wa Ripoti hii, Timu ya Ufuatiliaji wa malengo ya EFA duniani imetengeneza wavuti shirikishi mpya ambayo inaonyesha kiwango cha ukosefu wa usawa katika elimu ndani ya nchi. Hifadhidata ya Ukosefu wa Usawa Elimu Duniani (WIDE) inaweka pamoja na takwimu za karibuni kutoka kwenye Tafiti za Idadi ya Watu na Afya na Tafiti zinazotumia viashiria tofauti tofauti.

**Upana wa tofauti katika utajiri kwenye nchi zenye jitihada za kuandikisha watoto shuleni**

Vijana wenye umri kati ya miaka 17 na 22 ambao kiwango chao cha elimu ni chini ya miaka miwili, kulingana na utajiri, (%)





Kuchagua nchi tatu kwenye kanda ambazo ziko mbali zaidi katika kufikia malengo ya Elimu Kwa Wote – nchi za kiarabu, Afrika kusini mwa Sahara na Asia ya kusini na magharibi – mchoro unaonyesha kwamba tofauti za kiutajiri zipo takriban katika kila nchi yenye taarifa. Kwa kubofya vidoti vya kwenye tovuti, asimilia yenye athari inaonekana. Niger, nchi yenye tofauti kubwa, 88% ya vijana maskini zaidi wana elimu chini ya miaka miwili – maana yake wana umaskini mkubwa kielimu – ukilinganisha na 29% ya watu matajiri sana. Jordan, mwishoni mwa mchoro, ina tofauti ndogo sana. Matajiri au maskini, 1% tu ya watu wenye umri kuanzia miaka 17 hadi 22 ndiyo wenye athari zaidi za umaskini kielimu.

# Hifadhidata kuhusu Elimu (WADE)

Watembeleaji wa wavuti hii wanaweza kulinganisha makundi ndani ya nchi kulingana na viashiria mbalimbali vya elimu, na kulingana na sababu zinazohusiana na ukosefu wa usawa, zikijumuisha utajiri, jinsia, kabila, dini na mahali. Watumiaji wanaweza kutengeneza ramani, chati na majedwali kutokana na takwimu, kupakua, kuchapisha au kushirikishana kwenye mtandao. Wavuti imesanifiwa kwa kutumia vitu vya kushirikishana.

**Tofauti za utajiri zinakuzwa zaidi na tofauti za kijinsia**

Vijana wenye umri kuanzia miaka 17 hadi 22 wenye elimu chini ya miaka miwili, kulingana na hali ya utajiri na jinsia, Niger na Misri, (%)




Kwenye tovuti ya WEDE, mtumiaji anaweza kuangalia kwa kina katika vielelezo vinavokingamana vya madhara kwenye nchi zilizochaguliwa. Nchini Niger, matatizo siyo tu tofauti kubwa za utajiri bali matatizo hayo yanakuzwa na tofauti za kijinsia. Vijana wa kike maskini ndiyo wanaoathirika zaidi: 92% wanaonekana walisoma chini ya miaka miwili, ukilinganisha na 22% ya vijana wa kiume matajiri. Nchini Pakistan, pengo kubwa baina ya watu maskini linawaathiri vijana wa kike wanane juu ya kumi, ukilinganisha na kiwango cha chini ya vijana wa kiume watano juu ya kumi. Kwa ujumla, tatizo hili siyo kubwa sana nchini Misri, lakini pengo katika swala kijinsia ni kubwa mno: 36% ya vijana wa kike maskini wako katika ka hali ya umaskini wa kielimu uliyokithiri ukilinganisha tu na 2% ya vijana wa kiume matajiri.

www.education-inequalities.org

# Matumizi kwa ajili ya EFA: Mapungufu na fursa





Uzoefu wa muongo uliopita unaonyesha kwamba ongezeko la matumizi kwenye elimu bado una safari ndefu ili kufikia malengo ya Elimu kwa Wote. Lakini wakati idadi ya watoto wasioenda shule ikiwa imebaki pale pale, kuna ishara zenye kutia wasiwasi kwamba michango ya wafadhili inaweza pia kulegalega. Fedha pekee haziwezi kuhakikisha kwamba malengo ya EFA yanafikiwa, ingawa upungufu wa fedha unaweza kuwa na madhara. Juhudi mpya na za dhati za wafadhili zinahitajika kwa haraka. Wakati huo huo ni muhimu kuangalia fursa mpya ili kuziba pengo la fedha na kuboresha namna fedha za msaada zinavyotumika.

### *Matumizi zaidi ni muhimu*

Matumizi ya jumla ya serikali kwenye elimu yamekuwa yakiongezeka kwa kasi tangu mkutano wa Dakar. Ongezeko kubwa la matumizi limekuwa katika nchi maskini, ambapo lilikua kwa 7.2% kwa mwaka, kwa wastani, tangu mwaka 1999. Kwenye nchi za Afrika kusini mwa Sahara, ongezeko la mwaka lilikuwa 5%. Miongoni mwa nchi maskini na za kipato cha kati zenye takwimu, 63% ziliongeza sehemu ya pato la taifa linalotumika kwenye elimu kwenye muongo uliopita.

**Miongoni mwa nchi maskini na za kipato cha kati zenye takwimu, 63% ziliongeza sehemu ya pato la taifa linalo-tumika kwenye elimu**

Nchi nyingi zilizoongeza kasi ya kufikia malengo ya EFA katika kipindi cha muongo uliopita zilifanya hivyo kwa kungeza kwa kiasi kikubwa matumizi yao kwenye elimu au kudumisha kiwango ambacho tayari kipo juu. Kwa mfano nchini Tanzania, sehemu ya pato la taifa inayotumika kwenye elimu iliongezeka mara tatu, na kiwango cha uandikishaji elimu ya nsingi kiliongezeka mara mbili. Nchini Senegal, ongezeko la matumizi kutoka 3.2% ya pato la taifa hadi 5.7% lilisababisha ongezeko kubwa la uandikishaji kwenye elimu ya msingi na kuondoa tofauti za kijinsia.

Mbali na hali hii ya kutia moyo duniani, baadhi ya nchi bado zina safari ndefu ya kufikia malengo ya EFA, kwa mfano, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Guinea na Pakistani zimeendelea kuwa na kiwango cha chini cha matumizi, zikitumia chini ya 3% ya pato la taifa kwenye elimu. Pakistani ndio ya nchi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya watoto wasioenda shule – milioni 5.1 – ingawa ilipunguza matumizi yake kwenye elimu kutoka 2.6% hadi 2.3% ya pato la taifa kwa kipindi cha muongo uliopita.

Wasiwasi kwamba migogoro ya karibu ya kifedha na upungufu wa chakula ingeweza kuathiri maendeleo chanya ya matumizi kwenye elimu, inaonekana haukuwa na ukweli, ingawa madhara ya muda mrefu inabidi yatathminiwe.

Theluthi mbili ya nchi maskini na zenye kipato cha kati zenye takwimu ziliendelea kuongeza bajeti yao ya elimu wakati wa kipindi cha migogoro. Lakini baadhi nchi zilizo nyuma sana kwenye malengo ya EFA kama Chad na Niger, zilipunguza bajeti mwaka 2010 kutokana na kutokuwa kwa uchumi mwaka 2009.

Uchanganuzi mpya wa Ripoti hii unaonyesha kiasi ambacho baadhi ya nchi maskini zimefaidika na misaada. Katika nchi tisa, zote kutoka Afrika Kusini mwa Sahara, fedha za wafadhili ni zaidi ya robo ya matumizi ya serikali kwenye elimu (kielelezo 8). Kwa mfano, nchini Msumbiji, idadi ya watoto wasioenda shule ilipungua kutoka milioni 1.6 mwaka 1999 hadi chini ya laki tano mwaka 2010. katika kipindi hicho, misaada ilichukua 42% ya bajeti nzima ya elimu.

### *Je, misaada ya elimu imefikia kilele chake?*


Ongezeko kubwa la misaada kwenye elimu tangu mwaka 2002 lilikuwa mwaka 2009. kwa kiasi kikubwa lilichochewa na utolewaji wa mapema wa fedha zilizoahidiwa na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa ili kuzisaidia nchi maskini kukabiliana na madhara ya mgogoro wa kiuchumi. Ingawa misaada ya elimu ilibaki kuwa dola bilioni 13.5 mwaka 2010. Kati ya kiwango hicho, dola bilioni 5.8 zilikuwa kwa ajili ya elimu ya msingi (kilelezo 9). Wakati kiwango hicho kilikuwa mara mbili ya mwaka 2002-2003, ni bilioni 1.9 tu ilitengwa kwa ajili ya elimu katika nchi maskini. Hii haitoshi kuziba pengo la dola bilioni 16 zinazohitajika na nchi hizi. Misaada kwa elimu ya msingi kwenye nchi maskini iliongezeka na kwa dola milionni 14 mwaka 2010. Sio nchi zote zilifaidika kwa usawa. Ongezeko kati ya mwaka 2009 na 2010 lilikuwa zaidi nchi Afghanistan na Bangladeshi, ambazo zilipokea 55% ya fedha za ziada kwa kumi na sita maskini ambazo zilikuwa na ongezeko. Kwa upande mwingine, ufadhili kwenye nchi kumi na tisa maskini ulipungua.

Pamoja na ongezeko la misaada katika kipindi cha muongo uliopita, wafadhili walishindwa kutimiza ahadi yao waliyotoa wakati wa Mkutano wa G8 huko Gleneagles mwaka 2005 ya kuongeza misaada kiasi cha dola bilioni 50 ifikapo mwaka 2010. Afrika kusini mwa Sahara ilipata takribani nusu ya ongezeko lililoahidiwa. Dhana ya kwamba kiwango kama hicho kingeenda kwenye elimu kama kwenye miaka ya nyuma, kushindwa hkuo kulikuwa sawa na upungufu wa dola bilioni 1.9 kwa ajili ya shule kwa mwaka huo, au takribani theluthi moja ya misaada ya sasa kwenye elimu ya msingi.

Mchoro wa 8: Msaada katika elimu ni mgawanyo wa rasilimali kwa nchi maskini

Rasilimali za ndani na msaada kwa elimu,

Wastani wa nchi za kikanda zilizochaguliwa zenye kipato cha chini au cha kati, tangu mwaka 2004 hadi 2010




Zingatia: halama ya * inaonyesha kwamba mgawanyo maalum wa nchi katika msaada kutoka kwenye bajeti ulikadiriwa kutoka kwenye nyaraka za nchi; kuhusu nchi zingine, wastani wa 60% wa misaada ulifikiwa.

Chanzo: UNESCO (2012b)


Kinachotia wasiwasi zaidi, picha ya misaada kwa miaka kadhaa hadi mwaka 2015 haitii moyo. Mwaka 2011, jumla ya misaada ilipungua katika kiwango halisi kwa 3%. Hii ni kwa mara ya kwanza misaada ilipungua tangu mwaka 1997. Misaada ya bajeti ilipangwa kupunguzwa kama sehemu ya kubana matumizi kutokana na mtikisiko wa uchumi katika nchi tajiri. Kutoka mwaka 2010 hadi 2011, kiwango cha misaada kama sehemu ya pato la taifa kilipungua katika nchi kumi na nne kati ya ishirini na tatu wanachama wa Kamati ya Misaada ya Maendeleo ya OECD's.

Baadhi ya wafadhili wakubwa sio tu wanapunguza misaada yao kwa ujumla kwenye bajeti, lakini pia hawaipi Elimu kipaumbele, kitu ambacho kitapelekea misaada ya elimu kupungua kwa kasi sana kuliko viwango vya jumla vya misaada. Uholanzi moja ya wafadhili watatu wakubwa wa elimu ya msingi katika muongo uliopita, haichukulii tena elimu kama moja ya vipaumbele vyake na inatarajiwa kupunguza misaada kwenye elimu kwa 60% kati ya mwaka 2010 na 2015. Hii inaweza kuwa na madhara makubwa kwa baadhi ya nchi maskini. Uholanzi inatarajiwa kujitoa Burkina Faso, kwa mfano, wakati huo huo wafadhili wengine wanne nao pia wamesema wana nia ya kujitoa kwenye elimu kwenye nchi hiyo.

**Katika nchi tisa, zote kutoka Afrika Kusini mwa Sahara, fedha za wafadhili ni zaidi ya robo ya matumizi ya serikali kwenye elimu**

Mchoro wa 9: Msaada kwenye elimu ulituama mwaka 2010

Jumla ya misaada ya elimu iliyotolewa tangu 2002 hadi 2010




Chanzo: OECD-DAC (2012b).

Wafadhili wapya kama Brazil, China na India zimeanza kutupiwa jicho zaidi na zaidi. Lakini sio tu hazitoi kiwango cha kutosha cha misaada, bali pia hazitoi kipaumbele kwa misaada ya elimu ya msingi kwa nchi maskini.

### *Kutumia misaada kwa ufanisi*

Takwimu kuhusu elimu zinaonyesha sehemu tu ya hadithi nzima. Kuhakikisha kwamba fedha zinatumika kwa ufanisi ni muhimu sana. Miongoni mwa malengo thelathini kuhusu ufanisi wa misaada yaliyowekwa na OECD-DAC huko Paris mwaka 2005, ni moja tu lilifikiwa mwaka 2010 ambayo ni tarehe ya mwisho iliyokubaliwa.

Sekta ya elimu imekuwa sehemu muhimu ya agenda ya ufanisi wa misaada. Nchi Kenya, Msumbiji, Rwanda na Uganda, kwa mfano, kiwango kikubwa cha misaada kilichotolewa pamoja na mipango ya serikali ilichangia ongezeko la kujiunga na elimu ya msingi kuliko miaka ya nyuma.

**Nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa mfano, inakadiriwa kupoteza kiasi sawa na dola milioni 450 mwaka 2008**

Pamoja na jambo hili chanya, bado kuna hitaji la matumizi zaidi na mazuri ya misaada kwenye nchi maskini zaidi. Moja ya mambo muhimu kwenye kanuni za ufanisi kwenye misaada, Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Elimu (Zamani ukijulikana kama Mkakati wa Haraka wa kufikia malengo ya EFA), bado hayatumika. Ni mpango tu wa kukusanya fedha duniani kwa ajili ya misaada ya elimu, lakini ulitoa dola bilioni 1.5 tu kati ya mwaka 2003 na 2011, sawa na 6% ya jumla ya misaada yote kwenye elimu ya msingi kwenye nchi maskini na za kipato cha kati. Hiki ni kiwango kidogo kulinganisha na fedha zinazoenda kwenye sekta ya afya. Ushirikiano ulianzishwa sio tu kwa ajili ya kuongeza kiwango cha misaada, bali kuziba mapengo yaliyoachwa na serikali na wafadhili. Umuhimu wa ushirkiano ni kuhakikisha kwamba misaada inaratibiwa vizuri na mahitaji halisi yanafuatiliwa kwa ukaribu katika miaka ijayo ili kutoa taarifa za fedha baada ya mwaka 2015.

Na zaidi, wafadhili wanahitaji matokeo yanayoonekana kutokana na misaada yao kwa kuwa bajeti zimebana na kuna shinikizo kubwa la kuongezeka kwa uwajibikaji. Mkakati mpya ambao una lengo la kutoa misaada yenye kuzingatia matokeo inapelekea serikali za nchi zinazipokea kuwa na hali ya uwajibikaji zaidi ili kufikia malengo ya sera zao za elimu. Kwa mfano, Uingereza imeandaa mpango wa majaribio misaada ya ziada kuipa tuzo serikali ya Ethiopia kwa kila mwanafunzi wa ziada anayefaulu mtihani wa sekondari. Mkakati huu una hatari zake, hususani kwa nchi maskini ambazo haziwezi kugharamia gharama za kupata matokeo haya kama sababu za nje zinazuia mpango husika kufanya kazi vizuri.

### *Kubadilisha "laana ya rasilimali" kuwa baraka kwa ajili ya elimu*


Moja ya mambo yanayotatiza kwenye maendeleo ni suala la "laana ya rasilimali": nchi zilizobarikiwa kuwa na rasilimali zisizojizalisha tena, kama mafuta na madini, zimekuwa na kiwango kidogo cha ukuaji wa uchumi ukilinganisha na nchi zisizo na rasilimali. Nyingi kati ya hizi zina uwezekano mdogo wa kufikia malengo ya EFA na malengo mengine ya maendeleo. Lakini laana hii inaepukika kama rasilimali zitawekezwa kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Nigeria, moja wauzaji wakubwa nje wa mafuta na gesi, lakini ina idadi kubwa ya watoto wasioenda shule. Chad ilielekeza utajiri wake mpya uliogunduliwa kutoka kwenye sekta vipaumbele kama elimu na kuelekeza kwenye matumizi ya kijeshi. Nchini Liberia na Sierra Leone, kugombania maliasili ilikuwa kiini cha vita. Matumizi mabaya ya mapato yatokanayo na maliasili yanaweza kufikia hatua mbaya. Nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa mfano, inakadiriwa kupoteza kiasi sawa na dola milioni 450 mwaka 2008, kiasi hicho ni sawa na bajeti nzima ya elimu ya nchi hiyo na kinachotosha kupeleka shule ya msingi watoto milioni 7.2.

Maliasili kama zingegeuzwa kuwa mapato ya serikali na kutumiwa vizuri, zingeweza kusaidia nchi nyingi kufikia malengo ya EFA (kielelezo 10).

Mchoro wa 10: Mapato yanayotokana na mali asili yanaweza kukuza bajeti za elimu

Uwezekano wa ugharamiaji wa ziada kutokana na kuongeza kiwango cha juu cha mapato ya mali asili kuhusu jumla ya bajeti ya elimu mwaka 2010, nchi zilizochaguliwa, kwa malioni ya Dola za kimarekani




Zingatia: kuongeza kipato cha mali asili inakadiriwa kufanyika katika hatua mbili: (i) Ogezeko la mgawanyo wa mapato kutoka mauzo ya nje ya mali asili kufikia 30% kwenye madini na 70% kwenye mafuta: na (ii) fungu la 20% la haya mapato ya ziada kwenye elimu

Chanzo: Mahesabu ya timu iliyoandaa Ripoti ya ufuatiliaji wa Elimu Kwa Wote Duniani (2012) kutokana na Ghala –takwimu la UIS na mapitio ya makala ya IV ya Shirika la Fedha Duniani (IMF)

Botswana imegharamia elimu katika muongo uliopita kutokana na utajiri wa almasi ambao umeifanya kuwa moja ya nchi tajiri sana Afrika kusini mwa Sahara. Sio tu imeweza kufikia lengo la elimu ya msingi kwa wote bali pia kiwango chake cha uandikishaji elimu ya sekondari ni 82%, mara mbili ya wastani wa bara zima. Ghana imejenga maridhiano ya kisiasa kwa kuhakikisha kwamba utajiri wake unatumiwa kwa ufanisi, ikijumuisha uwekezaji kwenye elimu.

Uchanganuzi kwa ajili ya Ripoti hii unaonyesha kwamba kuna uwezekano wa kuongeza matumizi kwenye elimu katika nchi kumi na saba ambazo zina utajiri wa rasilimali au zinatarajia kuanza kuuza mafuta, gesi na madini. Kama mapato yatokanayo na maliasili hizi yakitumiwa vizuri na 20% ya rasilimali za ziada ikipelekwa kwenye elimu, zaidi ya dola bilioni 5 zinaweza kuzalishwa kwa mwaka kwa ajili ya sekta hiyo. Hii inaweza kugharamia elimu ya 86% ya watoto milioni 12 wa nchi hizi ambao hawaendi shule na 42% ya vijana milioni 9 ambao hawaendi shule. Nchi kadhaa pamoja na Ghana, Guinea, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Laos, Malawi, Uganda na Zambia zinaweza kufikia lengo la elimu ya msingi kwa wote bila kuhitaji misaada zaidi kutoka kwa wafadhili.

Ili kuhimiza matumizi ya haki na yenye tija ya mapato yatokanayo na maliasili, wanaharakati wa elimu inabidi waunge mkono hatua zenye kuhakikisha kwamba serikali zinazingatia viwango vya juu vya uwazi na utozaji kodi wa haki. Inabidi pia washirikishwe kwenye mijadala ya kitaifa kuhusu matumizi ya mapato yatokanayo na maliasili, kuchukulia elimu kama uwekezaji wa muda mrefu ili kupanua wigo wa uchumi na kuepuka laana ya rasilimali.

### *Kutumia fursa ya asasi binafsi*

Kutokana na hitaji kubwa la rasilimali kwa ajili ya kusaidia EFA na picha isiyoridhisha ya misaada ya kimataifa kwa ajili ya kuziba pengo hili, asasi binafsi zinaangaliwa kama chanzo mbadala cha fedha.

Makadirio yanaonyesha kwamba jumla ya michango yote ya asasi binafsi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa zaidi ya dola bilioni 50 kwa wastani mwaka 2008 na 2010, ukilinganisha na takribani dola bilioni 120 ya misaada rasmi. Ingawa kiasi kikubwa kilienda kwenye sekta ya afya. Kwa mfano, kwenye jumla ya misaada ilyotolewa na mashirika ya Marekani katika kipindi hicho, takribani 53% ilienda kwenye sekta ya afya na 8% tu ilienda kwenye elimu.

Uchanganuzi mpya uliofanywa kwa ajili ya Ripoti, kwa kutumia taarifa zilizopo kwa umma, unaonyesha kwamba asasi na mashirika binafsi yamekuwa yakichangia dola milioni 683 kwa mwaka kwenye elimu kwenye nchi zinazoendelea, kiasi ambacho ni sawa na 5% ya misaada ya elimu kutoka wafadhili wa DAC.

Takribani 20% ya fedha hizi zilitolewa na asasi ambazo malengo yake yanafanana na wafadhili wa asili. Ni asasi tano tu zilitathminiwa zilichangia zaidi ya dola milioni 5 kwa mwaka, kiasi ambacho ni sawa na misaada ya elimu kutoka ndogo wafadhili, kama Luxembourg au New Zealand (Kielelezo 11).


Vivyo hivyo, 71% ya michango kutoka kwenye mashirika ilitoka kwenye mashirika kama matano, kila moja likitoa zaidi ya dola milioni 20 kwa mwaka. Mengi ya mashirika yaliyochangia kiasi kikubwa kwenye elimu ni makampuni ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) au makampuni ya nishati.

Ni kiasi kidogo tu cha michango hii kilitumika kwa malengo ya EFA au kwa nchi ambazo bado ziko nyuma sana kufikia malengo ya EFA. Kuhusiana na kugharamia, elimu ya juu inapewa kipaumbele cha juu. Kuhusiana na eneo la kijiografia, mashirika – hususani yale ya sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano- hutilia mkazo mipango yao kwenye nchi za kipato cha kati kama Brazil, India na China, ambayo mara nyingi kimkakati wana faida nayo. Hata hivyo, mara nyingi, mikakati yao ni ya muda mfupi na iliyo gawanywa gawanywa.

**kiasi ambacho ni sawa na 5% ya misaada ya elimu kutoka wafadhili wa DAC.**

Mchoro wa 11: Ugharamiaji wa elimu kutoka mifuko mikubwa ya fedha inaonekana kutokana na misaada ya wafadhili

Michango kuelekea kwenye elimu kutoka Mifuko mitano mikubwa na misaada kabambe kutoka wafadhili wa serikali waliochaguliwa, 2009 – 2010 au miaka ya karibuni




Zingatia: Takriban theluthi mbili za wastani wa mwaka wa milioni 15 za dola za kimarekani kutoka William and Flora Hewlet Foundation, awali zilitoka kwa Bill & Melinda Gate Foundation. Mara nyingi, pesa za kusaidia elimu katika nchi zinazoendelea ilikadiriwa kwa kutumia taarifa kutoka mifuko ya fedha.

Vyanzo: kiambatishi, jedwali la 2 la misaada; Camegie Corporation ya New York (2011); Ford Foundation (2011); Master Card Foundation (2010); William and Flora Hewlett Foundation (2010); van Fleet (2012)

Asasi na mashirika kadhaa yametengeneza mikakati ya elimu bunifu ya yenye mafanikio katika nyanja za elimu ya awali, elimu ya msingi kuendeleza stadi za vijana na upimaji wa matokeo ya elimu. Hata hivyo, kwa ujumla ni vigumu kupima mafanikio yao: mara nyingi asasi binafsi hutoa kauli za kujisifu kuhusu ufanisi wa mipango yao bila kutoa taarifa za kutosha au tathmini za kutosha ya matokeo.

Ushiriki wa baadhi ya mashirika kwenye shughuli za EFA unawapa fursa kufanya ushawishi kwenye sera za umma katika namna ambazo zinaweza kuwapatia manufaa ya kibiashara. Wakati inaweza kuwa na faida kwa elimu, mikakati yao inabidi ichunguzwe kwa ukaribu kama ilivyo kwa misaada ya wafadhili.

**Asasi zote binafsi zinazo-taka kuchangia EFA inabidi zitoe taarifa kuhusu ahadi zao**

Kama hatua ya kwanza muhimu, asasi zote binafsi zinazotaka kuchangia EFA inabidi zitoe taarifa kuhusu ahadi zao, ikiwemo viwango vinavyotolewa na jinsi vinavyotumika. Hii itasaidia uchunguzi ili kuhakikisha maslahi ya kibiashara hayagongani na malengo ya jumla, wakati huo huo yakitoa taarifa kuhusu kiwango cha fedha kilichopo ili kuziba pengo la fedha kwa ajili ya EFA.

Michango yao itakuwa na ufanisi zaidi kama itaratibiwa na serikali na kuendana na mahitaji ya nchi. Muungano Biashara Duniani kwa ajili ya elimu kwa namna ya pekee ni njia yenye matumaini ya kusonga mbele kwa sababu unafanya kazi katika misingi ya malengo ya EFA


Njia nyingine ambayo asasi binafsi zinaweza kusaidia juhudi za serikali kuhusu elimu ni kuelekeza baadhi ya fedha zao kwenye mfuko wa pamoja. Mifuko ya afya duniani, kama Mfuko wa Duniani wa Kupambana na Ukimwi Kifua Kikuu na Malaria umekuwa na mafanikio katika suala hili. Lakini asasi kuu iliyopo kwenye sekta ya elimu “Global Partnership for Education” bado haijatimiza wajibu wake kikamilifu. Kwa wakati huu, sekta binafsi ina sauti kwenye kitengo cha sera cha asasi kupitia kiti chake kwenye bodi, bado ahadi za fedha zilizotolewa na asasi na mashirika kwenye mkutano wa asasi hazitaweza kutolewa kupitia mfuko wa pamoja.

### *Kuziba pengo*


Baada ya kipindi cha kuongeza bajeti za elimu, ambacho kimepelekea kuwe na matokeo ya aina yake, kipindi cha kutokuwa na uhakika kinatawala. Mtikisiko wa uchumi umeziathiri nchi tajiri, ukiwa na athari kwenye misaada kwa nchi maskini ambazo bado ziko mbali kuyafikia malengo ya EFA.

Kupungua kwa misaada kuna uwezekano wa kupanua pengo la matumizi kwenye elimu, hivyo masuluhisho yenye ubunifu yatahitaji kukabiliana na mapungufu. Misaada kutoka kwa wafadhili wanaochipukia kama Brazil, India na China ni chanzo kimoja cha fedha, lakini kwa sasa haijaelekezwa kwa kiasi cha kutosha kwenye nchi zenye mahitaji makubwa, hivyo vyanzo vingine vya fedha lazima vipatikane. Mapato yatokanayo na maliasili na asasi binafsi ni vyanzo viwili vya fedha, lakini ili michango hiyo iwe na ufanisi, mkazo zaidi inabidi uwekwe kwenye uwazi na kuendana na malengo ya EFA.





# Sehemu ya 2: Vijana na stadi: Kuiweka elimu kwa vitendo



*"Kama kuna mtu anaweza kunipa stadi na fursa ya kufanya kazi. Najua naweza kutimiza malengo yangu."*
-Kijana wa kike kutoka Ethiopia

Hitaji la kuendeleza stadi za kazi kwa vijana limekuwa jambo la haraka. Serikali sehemu mbalimbali duniani zinakabiliana na athari za muda za mrefu za mtikisiko wa uchumi na changamoto zinazoletwa na uchumi wenye uliojikita zaidi na zaidi kwenye maarifa. Ili nchi zikuwe na kustawi kwa kasi katika ulimwengu unaobadilika, inabidi zitilie mkazo zaidi uendelezaji wa stadi za nguvukazi. Na vijana wote popote wanapoishi bila kujali historia zao, wanahitaji stadi ambazo zitawaandaa kwa ajili ya kupata kazi bora ili waweze kupata ustawi na kushiriki kikamilifu kwenye jamii yao.

Hitaji muhimu za kuendeleza stadi kwa vijana lilitambuliwa kwenye lengo la tatu la EFA, likitilia mkazo "mahitaji ya kujifunza kwa vijana na watu wazima wote". Kutokana na kutoeleweka vizuri kwa lengo hilo na kutokuwa na uhakika wa jinsi ya kulipima, halijapata kipaumbele linachostahili kutoka kwa serikali, wafadhili na wadau wa elimu au sekta binafsi- na sasa limekuwa jambo muhimu kuliko wakati mwingine wowote.

Vijana ni wengi sana kuliko wakati mwingine wowote, na idadi yao inaongezeka kwa kasi sana sehemu mbalimbali za dunia. Kwenye nchi zinazoendelea pekee, idadi ya watu wenye umri kati ya 15 na 24 ilikuwa zaidi ya bilioni 1. Lakini ajira hazitengenezwi kwa kasi ya kutosha kukidhi mahitaji ya kundi hili kubwa la vijana. Kati ya watu wanane wenye umri kati ya 15 na 24 mmoja hana ajira. Vijana wana uwezekano mara tatu zaidi kuwa kutokuwa na ajira kuliko watu wazima. Wakati ukosefu wa ajira kwa vijana ukitarajiwa kuongezeka zaidi, vijana wengi wanakabiliana na uwezekano mkubwa wa kujikuta ajira za uhakika kwa miaka ijayo.

Ukosefu wa ajira unachukua nafasi kubwa kwenye ajenda, unapelekea watunga sera kuweka kipaumbele kwenye utengenezaji wa ajira kwenye makampuni binafsi. Wakati kuna mkazo kwenye suala hili, mahitaji ya mamilioni ya vijana wasio na stadi za msingi za kusoma na kuandika na kuhesabu yanaendelea kudharauliwa. Vijana hawa wanafanya kazi lakini wanapata malipo ya chini ya kiwango cha umaskini kwenye sekta isiyo rasmi mijini, au kwenye mashamba madogo katika hali kupungua kwa maeneo ya kulima. Sauti zao ni nadra kusikika kwenye maandamano. Kuwapa fursa ya kuepuka stadi za chini na kazi zenye malipo kidogo, inabidi kuwe msingi wa kila mkakati wa kuendeleza stadi.

Mara nyingi kumekuwa na hali ya kutokuwa na usawa kwenye kupata stadi, hii inazidisha athari kwa maskini, wanawake au watu kutoka kwenye kundi lililotengwa kijamii. Vijana ambao wamekulia kwenye umaskini na kutengwa wana uwezekano mkubwa wa kupata elimu ya chini au kuacha shule. Matokeo yake, wana fursa chache za kuendeleza stadi kwa ajili ya kupata kazi nzuri na hivyo kuwa katika hatari zaidi ya kutengwa kwenye soko la ajira. Ni kwa sababu hiyo Ripoti hii inaweka mkazo wa aina yake kwenye kutambua na kuelewa uwezekano wa vijana maskini kuendeleza stadi ambazo zitapelekea kupata ajira nzuri – kazi za uhakika ambazo zinalipa mishahara ya kutosha kununua chakula na kuweka akiba, kazi ambazo zinaweza kuwatoa kwenye umaskini.

Ripoti hii inatambua aina kuu tatu za stadi ambazo vijana wanahitaji
– stadi za msingi, zinazohamishika na za ufundi –
na katika mazingira ambayo wanaweza kujifunzia.

### *Stadi za msingi*

Katika kiwango cha msingi kabisa, stadi za msingi zinajumuisha stadi za kujua kusoma na kundika na kuhesabu ambazo ni muhimu kwa ajili ya kupata kazi ambayo inalipa mshahara wa kutosha kukidhi mahitaji ya kila siku. Stadi hizi pia ni sharti muhimu kwa ajili ya kuendelea na elimu na mafunzo, na kwa ajili ya kupata stadi zinazohamishika na za ufundi ambazo zinaongeza uwezekano wa kupata kazi nzuri.

### *Stadi zinazohamishika*

Stadi zinazohamishika zinajumuisha uwezo wa kutatua matatizo, kuwasilisha mawazo na taarifa kwa ufanisi, kuwa mbunifu, kuonyesha uongozi na kujitambua,na kuonyesha uwezo wa kijasiriamali. Watu wahitaji stadi hizi ili waweze kukabiliana na mazingira tofauti ya kazi na hivyo kuboresha uwezekano wao wa kubaki kwenye ajira zinazolipa.

**Kati ya watu wanane wenye umri kati ya 15 na 24 mmoja hana ajira**

*Stadi za kazi*

Kazi nyingi zinahitaji utaalamu malum, kutoka uzalishaji wa mbogamboga hadi kutumia mashine ya kushona, kutengeneza matofali au kutumia kompyuta.

"Njia za Kupata Stadi" zinaonyeshwa kwenye Ripoti hii zinaweza kuwa nyenzo ya kuelewa mahitaji ya kukuza stadi na maeneo ambayo sera inabidi iweke mkazo. Vijana wanaweza kupata stadi hizi tatu kupitia mfumo rasmi wa elimu na matawi yake pamoja na elimu ya ufundi. Vinginevyo, wale waliokosa elimu rasmi wanaweza kufaidika na firsa za kupata mafunzo kutoka kupewa nafasi ya pili hadi kupata stadi za msingi zinazoendana na kazi, zikijumuisha mafunzo kwa vitendo na yanayohusiana na kilimo.

***Vijana, stadi na kazi – kujenga misingi imara***

Katika nchi nyingi, kundi la vijana ndilo kubwa kuliko makundi mengine yote. Vijana hawa watakuwa msingi wa ukuaji kama nchi zitawapatia fursa. Lakini wengi hawaandaliwi kiasi cha kutosha kwa ajili ya jukumu hilo. Ukosefu wa usawa kwenye kupata elimu unawafunga vijana wengi, hususani vijana kutoka familia maskini, kwenye maisha magumu.

Kutoa fursa sawa ya elimu, na wakati huo huo kuongeza ubora wa elimu ni hatua ya kwanza muhimu kuhakikisha kwamba vijana wana stadi mbalimbali zinazohitajika kuboresha fursa ya ajira. Hata hivyo vijana wengi hawakupata fursa kama hizo. Vijana hawa wana uwezekano mkubwa wa kujikuta bila ajira au kufanya kazi zenye malipo madogo.



***Kundi kubwa la vijana linatoa changamoto***

*"Kila mwaka idadi ya vijana wasio na ajira inaongezeka, sio kupungua. Vijana wengi wanamaliza shule kila mwaka na hii inaongeza idadi ya vijana wasio na ajira wakati wa fursa za ajira ni zile zile."*

-kijana wa kiume kutoka Ethiopia

Takribani kijana mmoja kati sita duniani ana umri kati miaka 15 na 24. Wengi wao wapo katika nchi maskini kabisa. Kundi la vijana ndilo kubwa na linalokuwa kwa kasi sana katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara. Takribani theluthi mbili ya Waafrika wana umri chini ya miaka 25 ukilinganisha na chini ya theluthi moja kwenye nchi tajiri kama Ufaransa, Japan, Uingereza na Marekani. Ifikapo mwaka 2030, idadi ya vijana katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara itakuwa mara tatu na nusu zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1980. pia kuna idadi kubwa ya vijana wanaoishi katika nchi za Kiarabu na Kusini na Magharibi ya Asia, ambapo takribani nusu wana umri wa chini ya miaka 25.

Ili kuendana na ongezeko la idadi ya vijana kwenye nchi za Kiarabu, Kusini na Magharibi ya Asia na Afrika kusini mwa Sahara, ongezeko la ajira milioni 57 inabidi zitengenezwe ifikapo mwaka 2020 ili kuzuia ongezeko la ukosefu wa ajira kutoka kwenye viwango vya sasa.

Kwanza, serikali lazima zishughulikie suala la upungufu mkubwa wa stadi ambao unawaacha vijana wengi bila ajira au kunasa kwenye kazi za kijungu jiko. Kutengeneza ajira nyingi hakutatatua tatizo kama sehemu kubwa ya vijana hawatakuwa na stadi zinazohitajika kuzijaza.

***Ukosefu mkubwa wa usawa unawaacha vijana wengi bila stadi za msingi***

*"Kama nataka kuwa mtu mwenye maisha mazuri inabidi niendelee kusoma lakini kwa sababu za kiuchumi, siwezi kuendelea kusoma. Nilidhani ningeacha shule ili nisiwe mzigo na kulipia mahitaji yangu, lakini siwezi kupata kazi – je, ninawezaje kusoma?"*

-Kijana wa kiume kutoka Mexico

Ili kujiandaa kwa ajira, vijana wote wanahitaji stadi za msingi zinazopatikana kupitia elimu ambayo inayoendelea angalau hadi sekondari ya awali. Lakini nchi thelathini kati ya thelathini na tisa zilizofanyiwa uchanganuzi kwa ajili ya Ripoti hii, zaidi ya nusu ya vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 19 wanakosa stadi za msingi. Hali iko hivyo katika nchi ishirini na tatu kati ya thelathini za Afrika kusini mwa Sahara zenye takwimu

Sababu za stadi za msingi zinatofautiana, zikihitaji mikakati tofauti ya kisera. Nchini Burkina Faso, Mali na Niger, takribani vijana watatu kati ya watano hawajawahi kabisa kwenda shule wakati wanatimiza miaka kati ya 15 na 19, na hivyo wana uwezekano mdogo wa kupata fursa hiyo. Katika nchi nyingi za Afrika kusini mwa Sahara, wengi wa wanaoenda shule huacha kabla ya kumaliza elimu ya msingi. Nchini Rwanda, wakati wengi wana uzoefu wa elimu ya msingi, takribani nusu huacha shule kabla ya kumaliza elimu ya msingi.

Katika nchi nyingi maskini, idadi kubwa bado wako shuleni wakiwa na umri kati miaka 15 na 19, umri ambao walipaswa kuwa wawe wamemaliza walau elimu ya sekondari ya awali. Kwa mfano 35% ya ambao bado wako shule ya msingi katika umri huo, wana uwezakano mdogo wa kuendelea na ngazi ya juu ya elimu.

Hata katika nchi ambazo nusu ya wenye umri kati ya 15 na 19 wamemaliza elimu ya sekondari, kwa mfano India, Indonesia na Jamhuri ya Kiarabu ya Siria., kuna wengi ambao hawajahi kwenda shule, ambao waliacha na hawakumaliza elimu ya sekondari au ambao bado tu wapo katika shule ya msingi.

Umaskini ni kikwazo cha kupata elimu na stadi. Nchini Misri, mtoto mmoja kati ya watano kutoka familia maskini kabisa hajiungi kabisa na shule ya msingi, wakati karibu watoto wote kutoka tajiri hujiunga na elimu na sekondari.

Hata hivyo watoto na vijana wengi ambao hawaendi shule huwa wanafanya kazi. Mwaka 2008, inakadiriwa watoto milioni 115 wenye umri kati ya 5 hadi 17 walikuwa wanafanya kazi hatarishi sehemu mbalimbali duniani. Bila uwezo wa kupata stadi, wananaswa kwenye ajira zenye ujira mdogo na zisizo na uhakika kwa maisha yao yote.

Tofauti kati ya matariji na maskini zinaongezeka kadri watoto wanavyokuwa, ambapo wale kutoka familia maskini inabidi wachangie kipato cha familia. Nchini Colombia na Vietnam, karibu watoto wote wanaenda shule. Wakati vijana wengi kutoka familia tajiri wanafika sekondari ya awali, ni theluthi mbili tu kutoka familia maskini wanafikia hatua hiyo nchi Vietnam na takribani nusu nchini Colombia.


Katika nchi nyingi maskini, wasichana wana uwezekano mdogo wa kupata stadi za msingi kulinganisha na wavulana. Katika nchi maskini, tofauti kubwa za kijinsia zinatokea katika familia tajiri wakati fursa ni chache sana kwa wavulana na wasichana kutoka familia maskini. Nchini Burkina Faso, takribani 60% ya wavulana kutoka familia tajiri wanafika sekondari ya awali, ukilinganisha na 40% ya wasichana. Miongoni mwa familia maskini, 5% ya watoto wanafikia kiwango cha elimu ya sekondari ya awali, lakini idadai kama hiyo cha wavulana na wasichana wanafikia kiwango hicho cha elimu.

(Kielelezo 12).

**Niger, takribani vijana watatu kati ya watano hawajawahi kabisa kwenda shule wakati wanatimiza miaka kati ya 15 na 19**

Mchoro wa 12: Vijana wengi hawana uwezo wa kupata stadi za msingi

Hali ya elimu kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 19,kwa nchi, miaka ya hivi karibuni




Chanzo: UIS (2012a)

Kinyume chake ndio ukweli katika nchi za kipato cha kati, ambapo ubaguzi wa kijinsia unatokea miongoni mwa kaya maskini lakini vijana wengi kutoka kaya tajiri, wawe wavulana au wasichana, wana uwezo wa kupata stadi za msingi. Nchini Uturuki, kuna usawa wa kijinsia miongoni mwa familia tajiri, lakini kwa kaya maskini, 64% ya wavulana wanapata stadi za msingi kulinganisha na 30% ya wasichana.

Mahali ambapo vijana wanaishi kunabainisha fursa zao za elimu, ambapo tofauti za vijijini / mijini au mikoa zinaimarishwa na jinsia. Vijana wa kike wanaoishi kwenye maeneo ya vijijini wana uwezekano mkubwa wa kupata stadi za msingi. Nchini Pakistani idadi ya wenye miaka kati ya 15 na 19 waliofikia kiwango cha elimu ya sekondari ya juu iko juu mara mbili zaidi kwenye maeneo ya mijini ukilinganisha na maeneo ya vijijini. Karibu nusu ya wanawake wa vijijini katika nchi hii hawajawahi kwenda shule, wakati hali hii inawakabili 14% tu ya wanaume wa mijini. Huko Kerala, India, karibu kila mtu ana kiwango cha stadi za msingi lakini ni 45% tu wanapata fursa hiyo huko Bihar: 57% ya wavulana na 37% ya wasichana.

Tofauti hizo kwenye fursa bila shaka zinatokana na miundo ya umaskini, lakini zinaonyesha mgawanyo usio sawa wa rasilimali za serikali. Kwa mfano katika makazi duni nchini Kenye, watoto wengi hawana matumaini ya kupata stadi za msingi kwa sababu rahisi kwamba shule hazipo kwenye maeneo wanayoishi. Hii inaonyesha hitaji la kugawanya upya rasilimali ili vijana wasinyimwe fursa za kuingia kwenye soko la ajira kwa sababu ya hali yao ya utajiri, jinsia na mahali wanapoishi.

### *Vijana wanahitaji fursa ya pili ya kupata stadi za msingi za kusoma na kuandika na kuhesabu*

*"Kwa sasa kiwango changu cha elimu na stadi hakitoshi, lakini kama mikienda kwenye mafunzo siku za baadaye, naamini nitaweza kuzipata (stadi za msingi)."*

-kijana wa kike kutoka Ethiopia

Kiwango cha changamoto za kutoa fursa za pili kwa vijana wote wanaokosa stadi za msingi ni kikubwa kinavyojulikana kwa serikali. Ripoti ya mwaka huu ya Ufuatiliaji wa Malengo ya EFA inaonyesha kwamba katika nchi 123 maskini na za kipato cha kati, takribani vijana milioni 200 wenye umri kati ya miaka 15 na 24 hawajamaliza elimu ya msingi. Hii ni sawa na kijana mmoja kati ya watano. Kati ya hawa, 58% ni wasichana.

Kikanda, karibu mmoja kati ya watatu kwenye nchi za Afrika kusini mwa Sahara, na mmoja kati ya watano katika nchi za Kiarabu, wanakosa stadi za msingi kabisa. Zaidi ya nusu ya milioni 200 wanaishi katika nchi tano: Bangladeshi, Ethiopia, India, Nigeria na Pakistani. Wengi wa wanaokosa stadi za msingi wanaishi Kusini na Magharibi ya Asia (milioni 91) na Afrika kusini mwa Sahara (milioni 57).

Ingawa kuna programu nyingi bunifu zenye kutoa fursa ya pili sehemu mbalimbali duniani, nyingi kati ya hizo zinatolewa na Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), idadi ya vijana wanaofikiwa ni kidogo sana. Tathmini ya moja ya programu kubwa katika nchi saba inaonyesha kwamba zinawafikia watoto na watoto milioni 2.1. Wakati Ripoti hii inakadiria vijana milioni 15 katika nchi hizo saba wanahitaji fursa ya pili ya kupata stadi za msingi kabisa.

Suala la msingi ni kwamba njia ya gharama nafuu kabisa ya kutoa stadi za msingi ni kuhakikisha kwamba watoto wote wanamaliza elimu bora ya msingi na kuendelea na sekondari ya awali. Kwa kuwa hili bado halijafanyika kwa wengi, kuna hitaji la haraka la kuhakikisha vijana wote ambao wanakosa fursa, wanapata fursa ya pili ya kufikia lengo hili.

### *Stadi zinazohamishika: kuwaandaa vijana kwa ajili ulimwengu wa ajira*

*"(Shule) inakufundisha jinsi ya kuwasiliana na watu na jinsi mazingira ya kazi yanavyokuwa, kwa namna moja"*

-kijana wa kike kutoka Uingereza

**Kwenye nchi 123 zenye kipato cha chini na cha kati, takribani vijana milioni 200 wanahitaji nafasi nyengine ya masomo**

Waajiri wanataka uhakika kwamba vijana wanaoomba kazi angalau wana stadi imara za msingi na wanaweza kutumia ujuzi wao kutatua matatizo, kuchukua hatua na kuwasiliana na wafanyakazi wengine kuliko kufuata ratiba zilizoandaliwa. "Stadi hizi zisizohamishika" hazifundishwi kwenye kitabu cha darasani, lakini zinaweza kupatikana kupitia elimu bora. Ingawa waajiri mara nyingi wanaonyesha kwamba waajiriwa wapya kwenye soko la ajira wanakosa stadi hizi.

Ushahidi kutoka nchi tajiri unaonyesha kwamba kukaa shuleni kwa muda mrefu kunasaidia kuhakikisha kwamba stadi za kutatua matatizo zinapatikana. Nchini Canada, takribani 45% ya walioacha shule kabla ya kumaliza sekondari ya juu wanakosa stadi hizi, ukilinganisha na 20% ya wanaomaliza.

Elimu bora itaongeza pia hali ya kujiamini na hamasa. Stadi zinazohamishika, ambazo zinaweza kuwasaidia vijana kufanya kazi kwenye sekta isiyo rasmi katika nchi maskini na kuwa na mafanikio katika kazi zao zinaweza kuendelezwa kupitia elimu isiyo rasmi. Mengi inabidi yafanywe kwa vijana maskini ili kuendeleza stadi hizi. Kulitambua hili, Akanksha, NGO ya India, imeanzisha programu kwenye makazi duni ya Mumbai ili kuongeza hali ya kujiamini ya watoto maskini.

**Kulikuwa na takribani ajira milioni 29 pungufu duniani kwa mwaka 2011 kulinganisha na kabla ya mdororo wa kiuchumi**



Matokeo chanya nay a muda mrefu – vijana wanaoshiriki wanaonyesha maendeleo makubwa kwenye matokeo yao ya shule na vipato vyao.

***Kipindi cha hatari cha mpito kutoka shule hadi kazini***

*"Unatafuta kazi na wanakuuliza kama una cheti cha sekondari ya juu, lakini huna."*

-kijana wa kike kutoka Mexico

Vijana wengi wanapitia kipindi hiki kigumu cha mpito kutoka shuleni hadi kazini. Ugumu ambao vijana wanaupata katika soko la ajira inaonyesha ukosefu wa ajira na kazi zenye ubora wa chini - ikiwa pamoja na zenye usalama mdogo na ujira mdogo. Sababu zinazohusishwa na ukosefu wa elimu, kama vile umaskini, jinsia, ulemavu, mara nyingi yana uhusiano na hali ngumu katika soko la ajira. Hii sio bahati mbaya - ni kutokuwa na maendeleo sawa ya ujuzi, taratibu za kijamii na ubaguzi katika soko la ajira vikijumuishwa pamoja husababisha matokeo haya.

Baaadhi ya vijana, hususani katika nchi tajiri, wanakabiliwa na ukosefu wa ajira wa muda mrefu baada ya kumaliza shule. Takribani 13%a ya vijana duniani walihesabika kuwa hawana ajira mwaka 2011 – sawa sawa na vijana milioni 75, karibu milioni 4 zaidi kabla ya mgogoro wa kiuchumi duniani haujatokea mwaka 2007. Kwa wastani, viwango vya ukosefu wa ajira vilikuwa mara mbili hadi tatu zaidi kwa vijana kuliko watu wazima. Viko juu mara sita zaidi kwa vijana nchini Misri, na ni mara mbili na nusu nchini Afrika kusini, ni mara nne nchini Italia.

Ingawa inatarajiwa kwa vijana wana uwezekano mkubwa wa kutokuwa na kazi kuliko watu wazima kwa sababu wanasubiri hatua ya kuanzia, katika nchi nyingi vikwazo vya kupata kazi nzuri ni vingi kwa vijana wengi. Katikati ya miaka ya 2000, hata kabla ya kuanguka kwa uchumi duniani, 17% ya wenye umri kati ya miaka 15 na 29 nchini Italia hawakuwa na ajira kwa miaka mitano baada ya kumaliza shule.

Tangu kuanguka kwa uchumi duniani, fursa kwa vijana zimepungua, na kwa wale wenye elimu ya chini wameathiriwa sana. Kulikuwa na takribani ajira milioni 29 pungufu duniani kwa mwaka 2011 kulinganisha na kabla ya mdororo wa kiuchumi. Kwa mfano viwango vya ukosefu wa ajira nchini Hispania viliongezeka kati ya 2007 na 2009 hususani kwa wale ambao hawakumaliza elimu ya sekondari.

Hata hivyo, takwimu za ukosefu wa ajira hazitoi picha halisi ya tatizo linalowakabili vijana wengi. Zinaficha kweli kuwa vijana wengi waliacha kutafuta kazi kwa hawaamini kama wanaweza kupata. Watu ambao hawapo shuleni au kazini wala hawajishughulishi kutafuta kazi mara nyingi wanachukuliwa kama 'wavivu', ingawa kutojishughulisha kwao kunaonyesha hali halisi katika soko la ajira kuliko hamasa yao. Kama wale wanaojisikia kukatishwa tamaa ya kutafuta kazi wangehesabiwa. Viwango vya ukosefu wa ajira kwa vijana vingeongezeka sana, kwa mfano, mara mbili nchini Cameroon.

Mara nyingi wanawake wengi huchukuliwa kama hawajishughulishi. Tofauti ya kijinsia mara nyingi ni kubwa miongoni mwa vijana walioacha shule baada ya kumaliza elimu ya msingi. Nchini Jordani zaidi ya 80% ya vijana wa kike wenye elimu ya msingi pekee walikuwa hawajishughulishi kutafuta kazi kulinganisha na 20% ya vijana wa kike.

Mara nyingi vijana wa kike wanatumia muda mwingi kufanya kazi za nyumbani na katika sekta isiyo rasmi na hili halionekani kwa watunga sera. Uchanganuzi Ripoti hii kwa kutumia tafiti za hivi karibuni za nguvu kazi katika nchi tisa unaonyesha kwamba kuna vijana wa kike wengi zaidi ya wa kiume wanaochukuliwa kama hawajishughulishi katika nchi zote tisa, mara nyingi kwa kiasi kikubwa. Wanawake wachache kuliko wanaume hujaribu kutafuta kazi, mara nyingi kwa sababu ya mgawanyiko usio sawa wa kazi za nyumbani na ubaguzi katika ajira.

Wanawake wanaopata kazi mara nyingi hulipwa pungufu kuliko wanaume. Kwa wastani, nchini India na Pakistani, wanaume hupata 60% zaidi ya wanawake. Pengo la mshahara ni kubwa sana kwa wale wenye viwango vya chini vya stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Hata hivyo elimu bado inaweza kuleta tofauti kubwa katika mapato ya wanawake. Nchini Pakistani wanawake wenye kiwango cha juu cha kusoma na kuandika wanapata 95% zaidi kuliko wanawake ambao hawana stadi za kusoma na kuandika, ambapo tofauti ilikuwa 33% tu miongoni mwa wanaume.

Vijana wenye ulemavu wanakabiliwa na ugumu wa kupata elimu na kazi. Ni vijana wachache sana nchini Kenya wenye ulemavu wanasoma zaidi ya kiwango cha elimu ya msingi. Wanakumbana na vikwazo katika ajira kwa sababu ya viwango vyao vya chini vya elimu, kushindwa kuendana mazingira ya kazi na matarajio kidogo miongoni mwa familia na waajiri wao.

Vijana wengi hawana furaha kubaki bila ajira na wanalazimika kufanya kazi za kiwango cha chini ambazo si salama, zenye ujira mdogo na mara nyingi hufanya kwa masaa mengi. Kwa baadhi, hii ni inaweza kuwa msingi wa kupata kazi thabiti na inayoridhisha. Lakini kwa wengi kazi kama hizo ni kama mtego ambao ni mgumu kuukwepa.

Duniani, inakadiriwa vijana milioni 152 - na sawa na 28% ya vijana wote wanaofanya kazi - na wanalipwa chini ya dola 1.25 kwa siku. Katika nchi kama Burkina Faso, Cambodia, Ethiopia na Uganda, kufanya chini ya kiwango cha umaskini ni jambo lililoenea kuliko kutofanya kazi kabisa.

Vijana wana uwezekano mkubwa zaidi kuliko watu wazima wa kulipwa ujira mdogo. Mjini Ouagadougou, Burkina Faso, kwa wastani mapato ya watu wazima ni mara mbili na nusu ya vijana. Wakati vijana wanatarajia malipo yao kuongezeka kadri wanavyokua kiumri, kupata kipato cha chini ya kima cha chini ya mshahara kunawafanya wasiwe na fedha za kutosha kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Katika nchi maskini, vijana wenye elimu ndogo, ambao hawawezi kusubiri kupata kazi sahihi, wako katika hatari kubwa ya kupata ujira mdogo. Wakati hii inaweza kusababishwa na viwango vidogo vya elimu ambapo kuna vikwazo vingine katika kutafuta ajira inayolipa vizuri. Vile vile kuna uwezekano mkubwa kwamba viwango vidogo vya elimu mara nyingi ndio sababu kubwa ya vijana kufanya kazi zenye ujira mdogo. Nchini Cambodia kwa mfano 91% ya vijana wasio na elimu wanafanya chini ya kiwango cha umaskini, ikilinganishwa na chini ya 67% ya wenye elimu ya sekondari.

Vijana wanaoishi maeneo ya vijijini katika nchi maskini wana uwezekano mkubwa wa kuacha shule mapema na kufanya kazi zenye ujira mdogo kuliko kuwa bila ajira. Kwa mfano, katika maeneo ya vijijini nchini Cameroon, kiwango cha ukosefu wa ajira ni karibu 1%. Kilimo hutoa ajira kwa idadi kubwa ya vijana wenye elimu ya chini, lakini wengi wanalipwa kidogo mno. Theluthi mbili ya vijana wa vijijini wasio na elimu wanafanya kazi kwa ujira wa chini ya dola 1.25 kwa siku, ambapo wanawake wa vijijini na wasio na elimu hali yao ni mbaya zaidi.


Athari ya kumaliza elimu ya sekondari kwenye uwezo wa vijana wa kutafuta kazi zinazolipa vizuri unatofautiana kulingana na jinsia. Nchini Nepal, vijana wa kiume ambao hawajamaliza elimu ya sekondari wana uwezekano mkubwa wa kupata ujira mkubwa kulinganisha na vijana wa kike wenye elimu bora - zaidi ya 40% wanapata zaidi ya kiwango cha umaskini ukilinganisha na chini ya 30% ya vijana wa kike waliomaliza elimu ya sekondari.

***“Kuwekeza kwenye ujuzi kwa maendeleo***
*Kuna ukosefu wa elimu hivyo hatupati kazi na hatuwezi kuboresha maisha yetu. Hatuwezi kukuendelea.”*
- Kijana wa kiume kutoka India.

Kuendeleza ujuzi ni jambo la muhimu kwenye kupunguza ukosefu wa ajira, kutokuwa na usawa na umaskini na kuongeza ukuaji wa kiuchumi. Pia ni uwekezaji wa busara - kwa kila dola 1 inayotumika katika elimu inazalisha kati ya dola 10 hadi 15 kwenye ukuaji wa uchumi. Kama 75% ya wenye zaidi ya miaka 15 katika nchi 40 maskini duniani wangeweza kufikia kiwango cha chini cha nchi za OECD kwenye hisabati, ukuaji wa uchumi ungeongezeka kwa 2.1% kutoka katika kiwango cha chini na watu milioni 104 wangetoka katika lindi la umaskini uliokithiri.

Jamhuri ya Korea, imetoka kuwa maskini na kuingia kwenye utajiri ndani ya miaka thelathini, kwa kuweka mkazo na kupanga maendeleo ya ujuzi.Serikali iliboresha ujuzi wa watu wote kwa kufikia lengo la elimu ya msingi kwa wote halafu elimu ya sekondari kwa wote. Halafu ililenga kuvisaidia viwanda kwa kuendeleza ujuzi. Kwa kifupi serikali ilitoa mchango mkubwa ili kuweka uwiano kati ya ugavi na mahitaji ya ujuzi.

Baada ya miongo ya kuwa na ukuaji mdogo au kutokuwa na ukuaji kabisa, nchi za Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara zimeshuhudia ukuaji wa kasi katika miaka ya 2000. Zaidi ya theluthi moja ya nchi katika ukanda huu zimekuwa kwa kiwango cha 6% na kuna matumaini ya kuwa nchi za kipato cha kati katika nusu ya karne ya 21. Kutokana na uzoefu wa Jamhuri ya Korea na nchi nyingine za mashariki mwa Asia “tigers” unaonyesha kwamba ukuaji endelevu katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara utategemea sera nzuri za kiuchumi zilizoratibiwa na uwekezaji wa serikali katika elimu na ujuzi ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira.



**Kwenye nchi 123 zenye kipato cha chini na cha kati, takribani vijana milioni 200 wanahitaji nafasi nyengine ya masomo**

Serikali nyingi zimetelekeza ujuzi na maskini ndio waathirika wakubwa

Ingawa kuna ushahidi wa wazi wa thamani ya uwekezaji kwenye kukuza ujuzi, bado haupewi kipaumbele unaostahili. Katika uchanganuzi katika nchi arobaini na 46 zenye vijana wengi, wengi wao wakiwa na kipato cha chini na kati, zaidi ya nusu zimepiga au zinapiga hatua, baadhi zimeandaa nyaraka za sera zinazolenga kuendeleza ujuzi – mkakati wa mafunzo ya ufundi stadi au mkakati mpana wa kuendeleza ujuzi.

Wakati kuna mipango ya kuendeleza ujuzi, lakini mingi imegawanyika, hairatibiwi vizuri na haiendani kwa kiasi cha kutosha na mahitaji ya soko la ajira na vipaumbele vya maendeleo. Jukumu la kukuza ujuzi limegawanywa miongoni mwa mashirika kadhaa na uwajibikaji umepotea

Ukosefu wa mpango mkakati wa kukuza ujuzi, ikiwemo malengo ya kuwafikia maskini, inaonyesha mapungufu katika mikakati mingi ya maendeleo. Kati ya nchi arobaini na sita zilizofanyiwa uchanganuzi kwa ajili ya Ripoti hii, chini ya nusu zinashughulikia maendeleo ya stadi miongoni mwa vijana katika sekta isiyo rasmi. Hata hivyo, nchi chache zilitambua umuhimu na kujaribu kulishughulikia.

**Kuwaandikisha vijana wote hadi kiwango cha elimu ya sekondari ya awali utagharimu dola bilioni 8 kwa mwaka**

Kwa mfano, Ethiopia inafanya maendeleo ya stadi kama msingi wa mkakati kabambe na jumuishi wa ukuaji, kwa matumaini ya kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Inalenga kufakia lengo la elimu ya sekondari kwa wote ifikapo mwaka 2020 huku ikiweka mkazo katika stadi katika sekta ya kilimo na viwanda. Pia kuna mkazo mkubwa katika kuongeza tija katika uzalishaji wa makampuni madogo madogo ambapo vijana wengi maskini wanafanya kazi.

Karibu robo tu ya mikakati ya nchi iliyochanganuliwa inahitaji kuwajumuisha tena kwenye elimu ya mafunzo vijana ambao wameacha shule ya msingi. Kwa mfano, Sierra Leoni, iliandaa mpango thabiti wenye kuwalenga malengo mazuri ya mikakati ya ajira kwa vijana imelenga katika mafunzo ya ujuzi katika stadi ya ujasiliamari. Kwa muktadha huu ilikuwa karibu 57% ya umri wa maiaka 15 hadi 19 waliacha shule kabla ya kumaliza elimu ya sekondari ya awali, mkakati huu haukutoa kipaumbele cha kutosha kwa vijana ambao hawana stadi za msingi na hivyo wanahitaji programe za fursa ya pili ya elimu.

Ni mara chache vijana kuwa na uwezo wa kuchangia utengenezaji wa sera, lakini ni muhimu kwa sauti zao kusikika. Wale wenye umri kati ya miaka 15 na 24 wanafanya karibu moja ya sita ya idadi ya watu duniani, na mara nyingi hufanya sehemu yenye kubadilika badilika zaidi katika jamii, lakini pia ni yenye kuishi katika mazingira magumu zaidi na isiyo na nguvu. Wanaufahamu mkubwa wa hali halisi yao ya maisha kuliko watunga sera, ikiwa pamoja na uzoefu wa elimu na mafunzo na changamoto za kutafuta kazi nzuri. Hata pale ambapo vijana wanaalikwa kushiriki, sauti za maskini zina uwezekano mdogo wa kusikika. Mashauriano ya vijana huwa yanatawaliwa na vijana waliosoma na kutoka familia tajiri za mijini, wakati sauti za maskini walio wengi ni mara chache kujumuishwa.

Kuongeza fedha kutawapatia stadi vijana maskini

Kuna haja ya haraka kwa wafadhili kujikita kwenye maendeleo ya stadi kwa namna tatu: kwa kusaidia mipango ya nchi ili kuhakikisha vijana wote wanaweza kukaa shule angalau hadi kiwango cha elimu ya awali ya sekondari, kwa kusaidia mipango ya fursa ya pili kwa vijana ambao hawajawahi kupata fursa ya kupata stadi za msingi za kuandika, kusoma na kuhesabu na kwa kuwapa mafunzo vijana maskini ili kuboresha fursa zao za kupata mishahara mizuri.

Mkakati huu unahitaji fedha zaidi na malengo mazuri. Kuwaandikisha vijana wote hadi kiwango cha elimu ya sekondari ya awali utagharimu dola bilioni 8 kwa mwaka, kwenye nyongeza ya dola bilioni 16 inahitajika ili kufikia lengo la elimu ya msingi kwa wote ifikapo mwaka 2015. Wale wanaohitaji elimu na mafunzo mara nyingi wanatoka katika familia maskini, hivyo wao wenyewe hawawezi kumudu gharama. Serikali, kwa msaada wa hisani, inabidi ziongeze msaada ili kuhakikisha vijana wote wanapata fursa ya kupata stadi za msingi kwa kupitia mfumo rasmi au fursa za pili.

Ingawa, bila shaka, juhudi zaidi inabidi zifanywe, nchi nyingi maskini zimeongeza msaada wao kwenye sekta ya elimu katika kipindi cha muongo uliopita. Hata hivyo, matumizi kwenye elimu ya sekondari mara nyingi yanabanwa kwa faida ya elimu ya juu. Mbali na hiyo, baadhi ya wafadhili wanatoa msaada mkubwa kwa maendeleo ya stadi za msingi. Inakadiriwa dola bilioni 3 zilitumiwa na wafadhii mwaka jana kwa ajili ya maendeleo ya stadi, takribani 40% ya kiwango hicho kwa ajili ya elimu rasmi ya sekondari na mafunzo ya ufundi stadi.

Baadhi ya wafadhili wakiweka kipaumbele cha matumizi kwenye eneo hili, ambapo Ujerumani ikiwa inaongoza ikifuatiwa na Benki ya Dunia, Ufaransa na Japani. Baadhi ya wafadhili wadogo, kama Luxembourg na Uswisi waelekeza msaada wao wa sekta elimu kwenye kukuza stadi.


Nchi kama Japani zimetumia uzoefu wao wa ukuaji mkubwa wa uchumi kupitia maendeleo ya stadi. Sehemu kubwa ya ufadhili wa Ufaransa hauzifikii nchi zinazoendelea, ingawa, zaidi ya 60% ya dola milioni 248 ambazo Ufaransa ilitoa kwa elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi stadi mwaka 2010 zilikwenda kwa majimbo yake ya ng'ambo. Kuna maeneo mawili ya kuongeza ufadhili wa nje kwa ajili ya elimu: kugawanya upya fedha ambazo sasa zinatumika kwa ajili ya kutoa ufadhili kwa kuwapeleka vijana kutoka nchi zinazoendelea kusoma elimu ya juu katika nchi zilizoendelea, na kuwahimiza wafadhili wanaochipukia kujikita zaidi kwenye kukuza stadi, mkazo mkubwa ukiwa kwa vijana maskini.

mwaka 2010 zilikwenda kwa majimbo yake ya ng'ambo. Kuna maeneo mawili ya kuongeza ufadhili wa nje kwa ajili ya elimu: kugawanya upya fedha ambazo sasa zinatumika kwa ajili ya kutoa ufadhili kwa kuwapeleka vijana kutoka nchi zinazoendelea kusoma elimu ya juu katika nchi zilizoendelea, na kuwahimiza wafadhili wanaochipukia kujikita zaidi kwenye kukuza stadi, mkazo mkubwa ukiwa kwa vijana maskini.

Wakati elimu ya juu katika mazingira Fulani inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye kusaidia maendeleo ya ujuzi, bahati mbaya watu wachache katika nchi maskini wanafikia kiwango hicho. Mwaka 2012, kwa mara ya kwanza, OECD-DAC ziliwataka wafadhili kutoa taarifa ya kiwango cha misaada kilichotolewa kwa elimu baada ya sekondari ambacho kilienda kwenye ufadhili na gharama za kumgharamia mwanafunzi (gharama ambazo taasisi kwenye nchi wafadhili zinaingia zinapopokea wanafunzi kutoka nchi zinazoendelea). Takribani robo tatu ya misaada ya moja kwa moja inayoelekezwa kwenye elimu baada ya sekondari – sawa na karibu dola bilioni 3.1 – kilichotolewa mwaka 2010 zilienda kwenye vipengele hivyo (Kielelezo 13)

Mchoro wa 13: kwa baadhi ya wafadhili, sehemu kubwa ya "misaada" hairidhishi kwa nchi

Wafadhili wanne wa kwanza wanaotoa misaada ya moja kwa moja ya elimu kama fursa za kusoma nje na gharama zinahitajika kwa ajili ya wanafunzi, 2010




Zingatia: mchoro huu unaonyesha msaada ya elimu ya moja kwa moja, haionyeshi misaada ya elimu kutoka bajeti kuu
Chanzo: OECD-DAC (2012).

Mwaka 2010, karibu 40% ya misaada ya Japani kwenye sekta ya elimu ilienda kwenye ufadhili wa wanafunzi wanaosoma nchini Japani. Gharama inayotumika kumpatia ufadhili mwanafunzi mmoja kutoka Nepal anayesoma nchini Japani, ingeweza kuwasaidia vijana 229 kupata elimu ya sekondari nchini Nepal. Msaada uliotolewa na Ujerumani kwa ajili ya ufadhili wa masomo na gharama za kumgharamia mwanafunzi zilikuwa mara kumi na moja ya kiwango ilichotumia kwa ajili ya msaada wa moja kwa moja kwenye elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi stadi mwaka 2010. Msaada uliotolewa na Ufaransa kwa ajili ya ufadhili wa masomo na gharama za kumgharamia mwanafunzi zilikuwa mara nne ya kiwango ilichotumia kwa ajili ya msaada wa moja kwa moja kwenye elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi stadi mwaka 2010. Kama kiasi cha dola bilioni 3.1 kinachotumiwa kwa sasa na wafadhili kwa ajili ya wanafunzi kusoma kwenye nchi zao kingerudishwa katika nchi zinazoendelea, kingesaidia kushughulikia pengo kubwa la stadi za msingi.

Nchi zinazoibukia kama Brazil, China na India zinaweza kubeba jukumu kubwa kwenye misaada kwa ajili ya maendeleo ya stadi. Ili kufanya hivyo inabidi ziweke mkazo kwenye elimu na kuelekeza fedha zao kwa vijana maskini, zikijifunza kutokana na uzoefu wao wa kuhusianisha uwekezaji kwenye kukuza stadi na madiliko ya soko la ajira na kupunguza umaskini. Ni 2% ya msaada wa India wa takribani dola milioni 950 kwa mwaka kwa nchi nyingine zinazoendelea kutoka mwaka 2008 hadi 2010 ilielekezwa kwenye elimu. Kama ilivyo kwa wafadhii wengine wanaochipukia, sehemu kubwa itaelekezwa kwenye elimu ya juu ambayo maskini hawawezi kuipata.

Sekta binafsi pia inahitaji kuwekeza zaidi katika mafunzo ya stadi, kwa sababu itafaidika kwa kupata kutoka wafanyakazi wenye ujuzi na uwezo wa kuongeza tija na ushindani, kama viwanda nchini Ujerumani na Uswisi ambavyo vilivyowahusisha vijana katika mfumo wa mafunzo kwa vitendo vilivyogundua. Mashirika binafsi yanasaidia miradi bunifu. Hususani, MasterCard Foundation hutoa fedha kwa ajili ya mipango ya kuwasaidia vijana kupata stadi wazohitaji ili kupata ajira. Hata hivyo, kiasi
ambacho mashirika yanatoa kwa sasa kidogo sana ukilinganisha na ukubwa wa changamoto.

Pamoja na fedha kutoka vyanzo mbalimbali, lazima serikali ziratibu ili kufaidika zaidi na rasilimali hizi na kuhakikisha kwamba vijana maskini wanapewa kipaumbele. Moja ya njia za kuboresha matumizi ni kupitia mafunzo vizuri ya usimamizi wa fedha - kutoka vyanzo mbalimbali - ikiwa ni pamoja na kodi na ushuru kwenye makampuni, pamoja na fedha za misaada kutoka kwa wafadhili – ili serikali isimamie na kugawanya, wakati sekta binafsi inatoa mafunzo. Mfuko wa Ajira wa Nepal ni mfano mmoja wa mbinu za kupanua mafunzo kwa vijana maskini. Mahali ambapo fedha zimesimamiwa vizuri, matokeo yamekuwa chanya. Tunisia ilianzisha mfuko wa mafunzo mwaka 1999 na umefikia zaidi ya robo ya vijana wote wasio na ajira na kukuza stadi.

**Takribani robo tatu ya misaada ya moja kwa moja inayoelekezwa kwenye elimu baada ya sekondari - sawa na karibu dola bilioni 3.1 - kilichotolewa mwaka 2010**

### Elimu ya sekondari: inatengeneza njia ya kupata ajira

Elimu ya sekondari ni njia muhimu kwa ajili ya vijana ili kupata stadi ili kuboresha fursa zao za kupata ajira nzuri. Elimu bora ya sekondari ambayo inahusha uwezo wa aina mbalimbali. maslahi, na historia si tu inawaanda vijana kwenye njia ya kuelekea kwenye ulimwengu wa ajira, lakini pia ili kuzipa nchi nguvukazi iliyoelimika inabidi zishindane katika elimwengu wa leo unaondeshwa na teknolojia.

Duniani kote, vijana milioni 71 hawaendi shule. Hata katika nchi ambapo uandikishaji kwa ujumla ni wa juu, idadi kubwa wanaacha shule mapema (Kielelezo 14). Kwa wastani, 14% ya vijana katika nchi za Umoja wa Ulaya hawaendelei zaidi elimu ya awali ya sekondari. Nchini Hispania, kijana mmoja kati ya watatu huacha shule ya sekondari, ambayo ni sababu ya wasiwasi kutokana na athari kubwa za mgogoro wa kiuchumi na kiwango cha ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana ambacho ni 51% Machi 2012. umakini unahitajika katika nchi zote ili kuhakikisha elimu ya sekondari inahusiana na ulimwengu wa ajira.

**Duniani kote, vijana milioni 71 hawaendi shule**

### *Kuondoa vikwazo vya kupata elimu ya sekondari*

> *"Sikuwa na fedha kwa ajili ya vitabu na sare.*
> *Hali ya kifedha ya familia ilikuwa mbaya.*
> *Ilibidi niongeze kipato cha familia kwa*
> *kufanya kazi ajili ya ujira wa kila siku,*
> *kwa ajili ya maisha ya familia. Kupata fedha*
> *ilikuwa muhimu*
> *zaidi kwangu kuliko kwenda shule."*
>
> \- kijana wa kiume kutoka India

Katika nchi nyingi maskini ambazo zinahitaji kuongeza uandikishaji katika elimu ya sekondari ya awali, tatizo lililopo ni kuhakikisha kuwa watoto wanamaliza elimu ya msingi. Nchini Niger, ambapo moja ya tano tu ya wanaandikishwa katika elimu ya sekondari awali, uwiano wa walioandikishwa shule ya msingi ni 62% tu.

Kwa watoto ambao humaliza shule ya msingi, gharama za elimu ya sekondari zinaweza kuwa kikwazo. Shule za sekondari mara nyingi ziko katika maeneo ya mijini, ikiwa ni kikwazo kwa wale kutoka kaya maskini za vijijini ambao hawawezi kumudu gharama za usafiri. Vikwazo vya kijamii na kiutamaduni vinaweza kuzuia wasichana kuendelea na masomo mara wanapofikia umri wa ujana. Serikali inabidi zifanye mageuzi hususani kushughulikia vikwazo hivi, na hivyo kuwezesha vijana kuimarisha stadi za msingi.

Baadhi ya nchi za Afrika kusini mwa Sahara zimeongeza uandikishaji katika elimu ya sekondari ya awali kwa kuunganisha elimu ya msingi na elimu ya sekondari ya awali. Nchini Rwanda, kwa mfano, kuanzishwa kwa elimu ya msingi ya miaka tisa na kuondolewa kwa ada ya shule kwa sekondari ya awali mwaka 2009 iliongeza idadi ya wanafunzi wa sekondari ya awali kwa 25% ndani ya mwaka mmoja. Mbali na hivyo, mitaala iliandaliwa upya na kuweka mkazo kwenye masomo machache ya msingi, na mfumo mpya wa tathmini ulianzishwa.

Ada, iwe rasmi au isiyo rasmi, kwa kiwango tofauti inaathiri vijana kutoka familia maskini, ikiwazuia kujiandikisha na kuendelea na elimu ya sekondari. Kama hatua za kuondoa ada hazilengi kuwafikia maskini, zinaweza kuwafaidisha wasio maskini. Kenya ilifuta ada kwa shule za sekondari, kwa mfano, na kuongeza uandikishaji kutoka milioni 1.2 mwaka 2007 hadi 1.4 mwaka 2008. Serikali zilifidia shule kutoa dola 164 kwa kila mwanafunzi - mara kumi ya kiasi kilichopokelewa kwa kila mwanafunzi kwa shule za msingi. Kwa sababu watoto wachache maskini wanafikia elimu ya sekondari, wana nafasi ya angalau kufaidika na sera hii.

Vikwazo vikubwa vya kijamii, kiutamaduni na kiuchumi, kama vile ndoa za mapema, mara nyingi vinawazuia wanawake vijana kuendelea na masomo. Kuwa mama kunafupisha safari ya elimu kwa walio wengi, na wanakabiliana na vikwazo vikubwa kurejea shuleni. Zaidi ya mwanamke mmoja kati ya kumi wenye umri wa miaka kati ya 15 na 19 ni mjamzito au mama katika nchi za Afrika Kusini mwa Sahara, Amerika ya Kusini, na Asia ya Kusini, na kiwango kinaongezeka kwa idadi 30% au zaidi nchini Bangladesh, Liberia na Msumbiji


Hata pale ambapo sheria inalinda haki ya kupata elimu kwa vijana wa kike, juhudi zaidi inabidi zifanyike kwa kuwapa uwezo wa kufaidika na haki hiyo. Nchini Jamaica, shirika moja hutoa msaada, ikiwa ni pamoja na gharama za chakula na usafiri, ili kuwasaidia hususani wasichana na wanawake wajawazito maskini wenye umri chini ya miaka 16 kurudi tena shuleni baada ya kujifungua. Programu hizi zimeongeza uwezekano wa akina mama vijana wanaomaliza shule ya sekondari kutoka 20% hadi 32%.

### *Kufanya elimu ya sekondari iwe na uhusiano na ulimwengu wa kazi*

Elimu ya sekondari inapaswa kutegemea stadi za msingi na kutoa fursa sawa kwa vijana wote ili kuendeleza stadi zinazohamishika na za ufundi stadi ili kupata kazi nzuri au kuendelea na elimu. Mtaala mmoja wa elimu ya sekondari ya awali husaidia kuwapa watoto wote fursa sawa ya kuimarisha stadi za msingi. Wakati wanafunzi wako katika hatari kubwa ya kuacha shule wakiwekwa pamoja,

Mchoro wa 14: Baadhi ya vijana hata hawaanzi elimu ya sekondari, na wengi hua hawamalizi elimu hii

Kiwango cha uandikishaji wa jumla katika ngazi ya kwanza ya sekondari na hali ya maendeleo kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu katika elimu ya sekondari:




Zingatia: Kiwango cha maendeleo kulekea elimu ya juu ya sekondari ni kiashiria tosha cha maendeleo kutoka elimu ya kwanza ya sekondari hadi elimu ya juu ya sekondari. Imepimwa kutokana na sehemu ya kiwango cha uandikishaji wa jumla katika elimu ya juu ya sekondari hadi elimu ya kwanza ya sekondari. Katika mfumo unaoeleweka ambapo wanafunzi wotw wa elimu ya kwanza ya sekondari wanaendelea hadi elimu ya juu ya sekondari, kiwango kinalingana na 1. Honduras ina kiwango cha 75% cha uandikishaji wa jumla katika elimu ya kwanza ya sekondari na elimu ya juu ya sekondari ina kiwango cha 71%. Kiwango cha maendeleo kinakwenda hadi 95%, hali hii inaonyesha kwamba wengi wa wale ambao wana bahati ya kuingia shule za elimu ya kwanza ya sekondari wanaweza kundelea hadi elimu ya juu ya sekondari. Nchini Misri, kiwango cha uandikishaji wa jumla katika elimu ya kwanza ya sekondari ni 94%, na kiwango cha uandikishaji wa jumla kayika elimu ya juu ya sekondari ni 51%; kiwango cha maendeleo nchini Misri kuanzia elimu ya kwanza ya sekondari hadi ya juu inakadiriwa kuwa 0.54 (51/94). Hali hii inadhihirisha kwamba wakati vijana wengi wana fursa ya kuanza elimu ya kwanza ya sekondari, nusu yao tu ndiyo yenye uwezo wakuendelea na elimu ya juu ya sekondari.
Chanzo: Kiambatishi, jedwali la 7 la takwimu.

Matarajio ya chini, mazingira ya kujifunza yasiyovutia na athari za kundirika mara nyingi hupunguza mafanikio yao kwenye kujifunza. Kwa sababu hii, baadhi ya nchi maskini na za kipato cha kati, kama vile Botswana, Ghana, Afrika ya Kusini na Uganda, zimeandaa mtaala mmoja, pamoja na taratibu mpya za kufanya tathmini, vifaa vya kujifunzia na shughuli za mafunzo ya ualimu.

Katika ngazi ya sekondari ya juu, vijana wanahitaji kujifunza stadi zinazohamishika ili kurahisisha kipindi cha mpito kutoka shuleni hadi kazini, na stadi za ufundi stadi na kwa fani au sekta maalum za kazi. Kuchanganya stadi hiz zote kwa usawa na kuziandaa kutokana na mahitaji ya soko la ndani la ajira hutoa mtaala wenye uwiano unaoweza kuwanufaisha wote.



**Kusukuma wanafunzi wasiofanya vizuri kufanya mafunzo ya ufundi stadi kunaweza kuzidisha hali ya kutokuwa na usawa wa kijamii**

Kusukuma wanafunzi wasiofanya vizuri kufanya mafunzo ya ufundi stadi kunaweza kuzidisha hali ya kutokuwa na usawa wa kijamii na kupelekea katika waajiri kudharau programu hizi. Katika nchi kumi na nne kati ya ishirini na mbili katika utafiti PISA mwaka 2009, wanafunzi waliokuwa katika katika shule za ufundi walikuwa wa hali ya chini kijamii na kiuchumi, kwa wastani, kuliko wenzao katika elimu kwa ujumla. Katika nchi nne ambapo tofauti za matokeo zilikuwa kubwa sana kati ya wale walio katika elimu ya sekondari na wale wa ufundi stadi ambapo idadi ya wale kutoka familia maskini ilikuwa kubwa zaidi.

Uzoefu kutoka nchi za OECD unaonyesha kwamba wakati masomo ya ufundi stadi yakifundishwa sambamba na masomo ya kawaida na huyafanya yawe na uhusiano wa karibu na soko la ajira, viwango vya uandikishaji na kumaliza masomo vinaweza kuongeza.

Kuufanya mtaala rahisi kubadilika katika shule za sekondari za juu hususani katika suala la uchaguzi wa masomo na kuruhusu kurudi tena shuleni kunaweza kuwafaidisha wanafunzi wote, kama uzoefu Singapore ulivyoenyesha. Hata hivyo kuna baadhi ya vikwazo katika mkakati huu. Nchi nyingi zinazoendelea zinakosa rasilimali, vifaa na walimu wenye sifa ya kuleta mabadiliko hayo kwa ufanisi.

Baada ya Ghana kuanzisha mtaala mseto wa sekondari, idadi ya kozi za ufundi iliongezeka kwa asilimia 50% ingawa gharama ya kutoa kozi mpya ilikuwa karibu mara ishirini zaidi katika shule za vijijini kuliko za mijini ingawa ubora katika maeneo ya vijijini ni wa chini. Kama haiwezekani kutoa mafunzo na kusambaza walimu kwa ajili ya masomo ya ufundi stadi na kusambaza rasilimali kwa usawa, wanafunzi katika maeneo ya vijijini wanaweza kuishia kupata mafunzo yenye ubora wa chini.

### Kuimarisha uhusiano kati ya shule na kazi

> *"Kwenye vyuo na shule, inabidi wafanye zaidi, na sio ruhusa ya siku moja ambapo unaenda kufanya mazoezi kidogo ya kazi, inabidi wawe na siku mbili shuleni na siku tatu sehemu ya kazi, ili kuweka uwiano. Kwa hiyo upo shuleni, unajifunza unachohitaji kujifunza na unatoka kwa ajili ya kupata uzoefu."*
>
> *-kijana wa kike kutoka Uingereza*

Wanaomaliza shule mara nyingi wanaambiwa hawafai kwa kazi kwa sababu hawana uzoefu wa kazi. Kuhusianisha shule na programu zilizojikita kwenye kazi kupitia mafunzo kwa vitendo zinaweza kuwasaidia vijana kujifunza vitendo stadi za utatuzi wa matatizo -

na kufanyia mazoezi stadi muhimu za kazi. Mafunzo kwa vitendo yamethibitisha kuwa na mafanikio katika mazingira fulani. Muundo wa Ujerumani, kwa mfano, unajumuisha mafunzo yaliyopangiliwa kwenye kampuni na sehemu ya muda masomo darasani. Unafanya vizuri nchini Ujerumani kwa sababu ya kanuni imara na ushirikiano kati ya serikali ya waajiri na wafanyakazi.

Kwa sababu mara nyingi mafunzo kwa vitendo hupelekea kupata ajira, yanaweza pia kuwahamasisha vijana kukaa shuleni na kumaliza masomo yao. Nchini Ufaransa, kupitia mafunzo kwa vitendo huongeza uwezekano wa kuajiriwa miaka mitatu baada ya kumaliza

Mafunzo kwa vitendo yanaweza kuwa na faida hasa kwa maskini, lakini programu  za mafunzo zinaweza kuwa za kibaguzi. Nchi Uingereza, 32% ya vijana weusi na makabila mengine ya wachache hufanya mafunzo kwa vitendoi, ikilinganishwa na 44% ya vijana weupe. Wanawake wana uwezekano mdogo wa kupata mafunzo kwa vitendo, na wale wanaopata hulipwa 21% pungufu ya wanaume. Ushauri wa kazi unaweza kuwasaidia zaidi vijana maskini kupata na kukaa kwenye sehemu za mafunzo kwa vitendo, au kupunguza makali ya kipindi cha mpito kuelekea kwenye ajira kama uzoefu wa Japan ulivyoonyesha.

Mafunzo rasmi kwa vitendo ni vigumu sana kutekeleza katika nchi maskini, lakini yanaweza kufanya kazi katika mazingira fulani. Misri imeuchukuwa muundo wa Ujerumani na kuutumia kulingana mazingira yake, huku vyama vya biashara vikibeba jukumu kubwa kwa kutoa fursa za mafunzo. Theluthi moja ya wahitimu kutoka mpango huu waliweza kupata kazi mara moja na zaidi ya 40% iliendelea na elimu ya juu. Hata hivyo mifumo hiyo, inategemea sana imani kati ya serikali na waajiri, kitu ambacho si rahisi kukipata katika nchi nyingi maskini ambapo sekta isiyo rasmi ni kubwa.

### *Stadi zinazohamishika  kwa wote: Jambo la kuvutia lakini ni lengo lenye changamoto*

Stadi ambazo mtu anajifunza shuleni inabidi zipanuliwe zaidi ya maarifa ya somo husika. Kutumia maarifa kwenye mazingira halisi ya kazi, kuchambua na kutatua matatizo, na kuwasiliana kwa ufanisi na wenzake yote ni mambo muhimu katika kukuza stadi ambayo vijana wanahitaji kama wanataka kupata ajira nzuri katika uchumi wa dunia unaozidi kuendeshwa na teknolojia. Ikilitambua hili, baadhi ya nchi zinajitahidi kuingiza stadi zinazohamishika katika mitaala yao. Denmark, New Zealand na Hong Kong (China), kwa mfano, zote zinabainisha utatuzi wa matatizo kama kipengele muhimu katika mtaala.

Matumizi ya Teknohama katika elimu yanazidi kushika kasi duniani kote. Sio tu yanaboresha uzoefu wa kujifunza na kupunguza kiwango cha kuacha shule, lakini pia yawandaa vijana kwa kazi. Kompyuta inaweza kuwa ghali mno au adimu kwa baadhi ya shule, hasa katika nchi maskini, lakini redio na simu za mkononi zinaweza kufikia maeneo ya kijijini kabisa. Mafundisho shirikishi kwa kutumia redio, kama yanavyofanika nchini Honduras na Sudan Kusini, kwa mfano, yanatoa fursa ya kuboresha kujifunza kwa makundi ya pembezoni kwa gharama nafuu. Matumizi yake yameongeza ufaulu kwa hadi 20%

### *Kutoa njia mbadala kwa wale wanaoacha shule mapema*

Idadi kubwa ya vijana wanaacha shule kabla ya kumaliza elimu ya sekondari, hata katika nchi ya za kipato cha kati na cha juu. Wale wanaoacha shule mapema kuna uwezekano mkubwa ni kutoka katika kaya maskini. Msaada lengwa unahitajika ili kuwawezesha kuendelea na masomo yao ili waweze kupata sifa na stadi zinazohitajika kufaidika na fursa za ajira.

Nchini Uholanzi na Philippines, shule zimeanzisha mikakati rahisi ya kuwasaidia wale walio katika hatari ya kuacha shule, ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu kujiunga upya katika kipindi chochote katika mwaka wa masomo. Mjini New York City, ambapo moja ya tano ya wale wenye umri wa miaka 17-24 hawasomi wala hawafanyi kazi, programu mbili zinawalenga vijana walio katika mazingira magumu katika vitongoji vya karibu kwa kuwapa mafunzo kwa vitendo yenye ujira, ushauri binafsi na warsha. Mbinu hii imepelekea zaidi ya nusu kupata kazi ndani ya miezi tisa, na karibu moja ya tano walijiunga tena na kozi ili kujifunza stadi za msingi.

Mbinu mbadala za kujifunza stadi nje ya shule ya sekondari, kama vituo vya elimu ya masafa na vituo vya jamii vya mafunzo, inabidi viandaliwe kwa makini ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani la ajira na kusaidiwa na upatikanaji wa muda mrefu wa fedha. Stadi ambazo mtu anajifunza inabidi ziwe zinatambuliwa rasmi na waajiri.

Taratibu za kitaifa za utambuzi wa sifa zinaweza kuwapa waajiri taarifa juu ya mafunzo yaliyofanywa na vijana waliofuata njia mbadala za kujifunza. Kama zitaandaliwa kwa makini, zinaweza kubainisha kwa uwazi viwango vilivyogawanyika na mifumo ya utambuzi wa sifa iliyo nje mfumo rasmi  wa elimu ya sekondari. Hata hivyo siyo rahisi kutekeleza kwa ufanisi. Inahitaji ushirikiano wa karibu kati ya pande zinazohusika, ikiwa ni pamoja na serikali, taasisi za mafunzo, waajiri, na vyama vya wafanyakazi.

**Stadi kwa ajili ya vijana wa mijini:**
**Fursa kwa maisha bora ya baadaye**

Siku hizi idadi ya vijana wa mijini, kubwa kabisa katika historia na bado inakua, wakiwa wameelimika zaidi kuliko vizazi vilivyopita inawakilisha nguvu kazi kubwa kwa mabadiliko ya kisiasa, kijamii pamoja na ukuaji wa uchumi. Ikiwa ni matokeo ya ongezeko la asili na uhamiaji kutoka vijijini, inakadiriwa kuwa ongezeko la watu duniani litakuwa kubwa katika maeneo ya mijini miaka thelathini ijayo, ambapo watu wengi watakuwa wanaishi mijini kuliko vijijini katika maeneo yote ya nchi zinazoendelea ifikapo mwaka 2040.

***Maskini wengi wa mijini wanakosa stadi za msingi***

Ukuaji wa haraka wa miji umepelekea kuongezeka kwa umaskini wa mijini, unadhihirishwa na ukuaji wa makazi duni na makazi yasiyo rasmi. Mtu mmoja kati ya watatu leo hii anaishi kwenye makazi duni, ikiongezeka kutoka wawili watatu katika Afrika kusini mwa Sahara. Kwa ujumla, takwimu za karibuni zinaonyesha zaidi ya watu milioni 800 wanaishi kwenye makazi duni, idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka hadi milioni 889 ifikapo mwaka 2020. vijana wanachukua sehemu kubwa ya wale wanaoishi kwenye makazi haya. Mafunzo ya stadi na kazi yanaweza kuwapa mbadala wa mazingira duni ambayo wanaishi na kupambana ili kupata kazi nzuri.

Kiwango cha ukosefu wa elimu miongoni mwa watu maskini wa mijini mara nyingi kimekuwa kikisahaulika. Ukosefu wa usawa maeneo ya mijini mara nyingi ni mkubwa sana. – hii inamaanisha kwamba wanaoishi kwenye makazi duni sio lazima wawe wanaishi vizuri kuliko maskini wa vijijini – na ukubwa wa tatizo la umaskini mijini umekuwa ukipuuzwa.

Wakati fursa za elimu ni nyingi zaidi katika maeneo ya mijini kuliko vijijini katika nchi nyingi zinazoendelea, tofauti ya kupata stadi za msingi kati ya maskini wa mijini na vijijini sio kubwa. Katika nchi arobaini na tano maskini na za kipato cha kati, matajiri wa mijini wana uwezekano mkubwa wa kuendelea hadi mwisho wa elimu ya sekondari ya awali kuliko maskini wa mijini. Nchi kumi kati ya hizi, idadi ya wenye umri kati ya miaka 15 na 24 wanaokosa stadi za msingi ni kubwa zaidi, miongoni mwa maskini wa mijini kuliko maskini wa vijijini (Kielelezo 15)

Nchi Cambodia, kwa mfano, 90% ya vijana maskini wa mijini hawajamaliza elimu ya sekondari ya awali, ukilinganisha na 82% ya maskini wa vijijini na 31% matajiri wa mijini. Nchini Kenya, ambapo 60% ya wakazi wa Nairobi wanaishi kwenye makazi duni, viwango vya chini vya elimu rasmi miongoni mwa vijana kutokana na ukosefu wa shule za sekondari katika makazi duni vinawanyima fursa za kupata kazi nzuri.


***Ajira nyingi za vijana maskini wa mijini ziko kwenye sekta isiyo rasmi***

> *"Ni ngumu sana kupata kazi ya muda mrefu.*
> *Muda mrefu zaidi wa kufanya hauzidi wiki moja.*
> *Na kwa kazi yangu napata birr 30 (dola 1.70) kwa siku."*
>
> \- Kijana wa Ethiopia

Ukosefu wa stadi na elimu kwa maskini wa mijini unawaacha wengi wanaofanya katika biashara ndogo ndogo katika sekta isiyo rasmi bila kumbukumbu za biashara, hadhi ya kisheria au kanuni.

Mchoro wa 15: Tofauti kubwa kati ya watu matajiri na maskini washio mjini

Asilimia ya vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24 wanaoacha shule bila kumaliza elimu ya kwanza ya sekondari, kwa kuzingati utajiri na mahali, nchi zilizochaguliwa, miaka ya hivi karibuni




Chanzo: UIS (2012a)

Kazi katika sekta isiyo rasmi zinajumuisha shughuli za kujikimu, kama kuzoa uchafu na biashara za mtaani, pamoja na kushona na kutengeneza nguo, kutengeneza magari, ujenzi, kazi za shamba, kazi za sanaa. Zikiwa sio rasmi na hazifuati sheria, mara nyingi kazi hizi zina malipo madogo, hazina uhakika na zinafanyika katika mazingira mabaya.

Wakati idadi kubwa ya watu duniani walionaswa kwenye hali ngumu, na kazi zisizofuata sheria ni ngumu kuipima kwa usahihi, Shirika la Kazi la Duniani (ILO) inakadiria wapo bilioni 1.53. Sekta isiyo rasmi inachukua 70% ya ajira zisizo za kilimo katika baadhi ya nchi za Afrika kusini mwa Sahara, na zaidi ya nusu katika nchi maskini za Amerika ya Kusini. Vile vile ni ajira kuu kwa wafanyakazi wengi wa kusini na magharibi ya Asia.

Ubaguzi kwenye elimu na na masoko ya ajira huwanyima fursa baadhi ya makundi. Vijana katika mazingira tofauti wanakabili-ana na ugumu wa kuendelea na kupata elimu na mafunzo, pamoja na kazi zenye ujira, wakati huo huo wakikabiliana na mzigo mzito wa kazi za nyumbani zisizo na ujira. Wanawake wengi ukilinganisha na wanaume wameajiriwa kwenye sekta isiyo rasmi au isivyo rasmi kwenye sekta rasmi katika nchi ishirini na tano kati ya thelathini na tisa kwa mujibu wa utafiti wa karibuni wa ILO. Kazi nyingi zinazofanywa na wanawake zina vikwazo : nyingi zinafanyika nyumbani, na wanawake ni wengi sana kwenye shughuli zisizo rasmi na zisizo salama, kama uzoaji wa taka na biashara za mitaani. Wakiwa kazini, wana uwezekano mkubwa wa kulipwa kidogo kulinganisha na wanaume. Huko Buenos Aires, kwa mfano, wanawake kwenye makampuni yasiyo rasmi wanapata malipo ya 20 kidogo kuliko wanaume.

Sekta isiyo rasmi inaweza kuwa fursa yenye kuvutia zaidi wakati vijana wana stadi stahiki. Wafanyakazi kwenye sekta isiyo rasmi katika miji mikuu saba ya Afrika magharibi ambao wamemaliza elimu ya msingi au sekondari ya awali mara nyingi wanaweza kupata 20% hadi 50% zaidi kuliko wasio na sifa hizo. Lakini wengi wanaoingia kwenye sekta isiyo rasmi wanakosa stadi za msingi. Nchini Rwanda mwaka 2006, 12% tu ya wale wanaofanya kazi kwenye sekta isiyo rasmi walikuwa na elimu zaidi ya sekondari ya awali, ukilinganisha na 40% kwenye sekta rasmi.

### Kuongeza fursa za mafunzo kwa vijana wanaoishi kwenye mazingira magumu

Kadri athari za mtikisiko wa uchumi zinavyoendelea, idadi ya vijana wanaopata ujira chini ya kiwango cha chini cha umaskini wanaofanya kazi zisizo za ujuzi katika sekta isiyo rasmi inaongezeka. Inabidi wawe sehemu kuu ya mikakati ya kitaifa ya kukuza stadi, ingawa mara nyingi hali haiko hivyo. Utafiti uliofanyika kwenye nchi arobaini na sita zinazoendelea kwa ajili ya Ripoti hii unaonyesha kwamba nyingi hazina mkakati wa taifa wa kuendeleza stadi ambao unashughulikia kinagaubaga sekta isiyo rasmi mijini.

India, moja ya nchi chache zinazotilia mkazo suala hilo, imeandaa mkakati kwa ajili ya wafanyakazi wasio kwenye sekta rasmi. Pia ina Sera ya Taifa ya Wafanyabiashara wa Mitaani ambayo inasema kwamba, kwa kuwa wafanyabiashara milioni kumi wa mitaani wanaendesha viwanda vidogo vidogo, inabidi wapate mafunzo ili kuboresha stadi zao za ufundi na biashara ili waweze kuongeza kipato chao na kutafuta kazi mbadala.

Mipango inayotoa fursa ya pili ni muhimu ili kuwapa maskini wa mijini stadi za kusoma na kuandika na kuhesabu. Ingawa kuna mikakati bunifu inayofanywa na NGO, fursa za pili kwenye sehemu za dunia ambako zinahitajika sana mara nyingi ziko katika kiwango kidogo. Mara nyingi haziratibiwi vizuri, na serikali ina taarifa kidogo kuhusu shughuli zao.

Kuongeza stadi za msingi kwa wale wenye umri kati ya miaka 15 na 24, na kuziunganisha na mafunzo ya ufundi, inaweza kuwasaidia kupata kazi. Mradi wa Mafunzo kwa Ajira nchini Nepal kwa ajili ya vijana ambao hawasomi ni moja ya mipango hiyo. Umepata mafanikio makubwa ya kuyafikia makundi ya pembezoni – 66% ya wanafunzi kutoka jamii za madaraja ya chini na makabila madogo madogo. Utafiti wa kufuatilia wahitimu 206 wa mradi huo, unaonyesha kwamba 73% walipata ajira.

Njia nzuri ya kuendesha mafunzo ya stadi ni kuyaunganisha na taasisi ndogo ndogo za kifedha au mipango ya hifadhi ya jamii ambayo itawasaidia walengwa wake kuondokana na umaskini katika kipindi kifupi. Chile Solidario iliyoanzishwa mwaka 2002, inatoa huduma za uhamishaji fedha pamoja na aina nyingine za msaada, ikiwemo fursa ya upendeleo ya kupata mafunzo yenye lengo la kuongeza uwezo wa kuajiriwa, mkazo ukiwa kwa wanawake maskini wenye kiwango kidogo cha elimu na uzoefu mdogo au kutokuwa na uzoefu kabisa wa kazi. Ajira ziliongezeka kwa asilimia nne hadi sita miongoni mwa wanawake waliojiunga na mpango huu mwaka 2005, kwa kiasi fulani ni kutokana na ongezeko la ushiriki kwenye programu za mafunzo.

Programu zinazotoa mafunzo ya darasani na uzoefu wa kazi kwenye stadi maalum na za msingi, pamoja na stadi za maisha, msaada wa kutafuta kazi, ushauri nasaa na taarifa zinazooengeza uwezekano wa kuajiriwa, zimekuwa na mafanikio katika sehemu mbalimbali za dunia, hususani Amerika ya Kusini na Carebbian. Programu hizi zinawalenga vijana maskini wa mijini, hususani vijana wa kike, zikiwa na mafanikio ya kiasi fulani. Nchi Colombia mishahara ya wanawake waliomaliza programu ya Jovenes en Accion iliongezeka kwa wastani wa 20%.




Fursa zao kwenye ajira rasmi nazo ziliongezeka ikiwa ni matokeo ya kuchanganya mafunzo ya darasani na mafunzo ya kazini katika mazoezi mbalimbali ambayo yana uhusiano wa karibu na mahitaji ya soko la ajira. Nchini Peru, programu ya PROJoven iliongeza fursa za wanaume kupata kazi kwa hadi 13% na wanawake kwa hadi 21%.

Programu nyingi za Jovenes katika nchi za Amerika ya Kusini zimeingizwa katika taasisi za taifa za mafunzo au nafasi yao kuchukuliwa na mikakati kama hiyo, hususani Entra 21. Zinatoa mifano ya kuigwa kwa nchi nyingine, zikiwemo nchi za Kiarabu, zikionyesha kwamba mipango mahususi inaweza kuongeza fursa za ajira kwa vijana kutoka familia maskini. Inaweza kuwa na gharama, na kuhitaji makampuni ya kutosha yenye uwezo wa kushiriki, kinaweza kuwa kitu kisichowezekana katika maeneo ya Afrika kusini mwa Sahara, kwa mfano, mahali ambapo idadi ya ajira kwenye sekta rasmi ni ndogo.

### Zaidi ya stadi za msingi kwa ajili ya vijana maskini

Wakati vijana wa mijini wanapokuwa wamepata stadi za msingi, serikali inabidi ziweke mkazo kwenye na kusaidia mafunzo ya stadi zinazohamishika na za ufundi, hususani kwenye biashara ndogo na za kati katika sekta isiyo rasmi ambayo ina fursa ya kukua. Njia ya mafunzo kwa vitendo ni moja ya mbinu zinazoweza kuwafikia idadi kubwa ya vijana walioajiriwa katika sekta isiyo rasmi. Inaweza kuwa ya gharama nafuu, kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na hali ya halisi na mara nyingi hupelekea kupata ajira.

Ni muhimu, kuhakikisha kwamba upatikanaji wa mafunzo kwa vitendo unakuwa katika usawa. Nchi Ghana ni 11% tu ya asilimia ishirini ya watu maskini walifanya mafunzo kwa vitendo ulinganisha na 47% ya matajiri. Vivyo hivyo mafunzo kwa vitendo mara nyingi yanakuwa katika fani ambazo zinapatikana zaidi kwa wafanyakazi wanaume na sio kwa wanawake.

Mabadiliko yenye lengo la kabadilisha mfumo wa asili wa mafunzo kwa vitendo na kuwa mfumo wa mafunzo kwa vitendo wa aina mbili yalifanyika kati ya mwaka 1990 na 2000 katika nchi mbalimbali, zikiwemo Benin na Togo. Yanajumuisha mafunzo ya nadharia na vitendo. Mbinu hii inahitaji makubaliano kati ya serikali, makundi yanayowakilisha wafanyakazi kwenye sekta isiyo rasmi na wanaofanya kazi za mikono wanaotaka kufanya mafunzo kwa vitendo. Kama yakitekelezwa kwa mafanikio, mafunzo kwa vitendo ya aina mbili yanaweza kuwa sehemu yenye ufanisi na endelevu ya mifumo ya taifa ya mafunzo ya ufundi. Kwa mfano, chini Burkina Faso, gharama za mabadiliko ya mafunzo kwa vitendo zilikuwa theluthi moja kama kozi za mafunzo rasmi.

Taratibu utambuzi wa mfumo wa asili wa mafunzo kwa vitendo kama suala rasmi inaweza kuwa chaguo rahisi la kisera kuliko kuyabadilisha yote kabisa na kuwa mafunzo kwa vitendo ya aina mbili kwa nchi zenye uwezo mdogo wa kitaasisi, kama uzoefu wa Cameroon na Senegal unavyoonyesha. Mikakati kama hiyo inaweza kuwa yenye ufanisi kama itaandaliwa na kutekelezwa kwa ushirikiano kati ya vyama vya sekta isiyo rasmi na asasi nyingine za kitaaluma.

Uingizaji taratibu wa hadhi rasmi inaweza kujumuisha kanuni ili kuwalinda wanaofanya mafunzo kwa vitendo ili wasinyonywe, wasiwasi wa kawaida katika mifumo ya asili. Inajumuisha viwango vya juu vya masaa ya kazi kwa siku na kwa wiki, ukomo wa idadi ya miaka ya mafunzo kwa kila aina kazi na hatua za usalama. Kuthibitisha stadi za wafanya mafunzo kwa vitendo na uzoefu wa kazi kupitia utaratibu wa kitaifa wa kutambua sifa za kitaaluma inaweza kuongeza zaidi thamani ya mafunzo haya na kuongeza uwezekano wao wa kuajiriwa.

Njia nyingine ya kazi za kujikimu ni ajira binafsi. Vijana wengi katika maeneo ya mijini katika nchi za Kiarabu na Afrika kusini mwa Sahara wanaiona hii kama fursa ya uhakika. Mwaka 2008, utafiti uliofanyika Misri ulionyesha kwamba takribani 73% ya vijana wangefurahi kama wangekuwa wajasiriamali. Hata hivyo, stadi za ujasiriamali zinakosekana miongoni mwa vijana maskini wa mijini.

Uzoefu wa Bosnia na Herzegovina na Ghana unaonyesha kwamba matokeo ya mafunzo ya ujasiriamali hupungua kama washiriki hawana stadi za msingi na hawana uwezo wa kupata aina nyingine za msaada, ikiwemo rasilimali zinazohitaji kuanzisha biashara, za kuwawezesha kutumia stadi zao mpya walizopata.

Uandaaji wa mtaala wa mafunzo ya ujasiriamali yanayowalenga vijana maskini wa mijini, unahitaji kutilia mkazo mafunzo ya stadi za msingi za kusoma na kuandika na kuhesabu zikiunganishwa na rasilimali zinazohitajika kuwapa vijana fursa nzuri ya kufanikiwa.

### Stadi kwa ajili ya vijana wa vijijini – njia ya kuepuka umaskini

> *"Natokea kijijini. Inajulikana kwamba elimu haipewi kipaumbele katika maeneo ya vijijini ; familia haziimizi watoto wao kwenda shule. Nilianza kujisomea mwenyewe kwa sababu nilikuwa na shauku. Lakini ili kuwa mwanafunzi unahitaji vifaa vya kujifunzia na sikuweza kumudu gharama zake."*
>
> -kijana kutoka Ethiopia

Maskini walio wengi – 70% au takribani watu bilioni 1- wanaishi katika maeneo ya vijijini, hususani katika nchi maskini na zenye kipato cha kati. Wengi wapo katika nchi za Afrika kusini mwa Sahara na kusini mwa Asia, ambapo wengi wao wanategemea mchanganyiko wa kilimo kidogo, vibarua vya msimu na shughuli ndogo ndogo za ujasiriamali zenye kipato kidogo. Kadri idadi ya watu duniani inavyoendelea kuongezeka na hitaji la hitaji la chakula linaongezeka wakati ardhi inazidi kuwa haba, kukuza stadi ni muhimu sana ili vijana kwenye maeneo ya vijijini waweze kutumia teknolojia mpya kwenye kilimo, na kuwa na fursa kubwa za kazi zisizo za shamba.

### *Kwenye maeneo ya vijijini, vijana wa kike wana hali ngumu zaidi kuliko vijana wa kiume*

Katika maeneo mengi ya vijijini vijana maskini, hususani wa kike, wanakosa stadi za msingi, na kuwafunga vijana kwenye kazi za kujikimu. Tofauti ya kijinsia inaonekana zaidi kwenye nchi ambazo watu wengi hawajamaliza elimu ya sekondari ya awali. Nchini Benin, Cameroon, Liberia na Sierra Leone, takribani 85% ya vijana wa kike wa vijijini wakosa stadi za msingi, ukilinganisha na chini 70% ya vijana wa kiume. Hata nchini Uturuki, nchi ya kipato cha kati, tofauti ya kijinsia katika maeneo ya vijijini ni kubwa – 65% ya vijana wa kike hawamalizi elimu ya sekondari ya awali, ukilinganisha na 36% ya vijana wa kiume (Kielelezo 16).


Sio tu wanawake wana viwango vya chini vya elimu, lakini pia wana rasilimali chache na wana uwezo mdogo wa kuhama. Mara nyingi wanaachwa nyuma na kufanya kazi zinazohitaji ujuzi wa chini ambazo wengine hawataki kuzifanya.

Kuboresha elimu na stadi za vijana katika maeneo ya vijijini, hususani vijana wa kike, sio tu itaongeza fursa zao, lakini pia itaongeza tija yao, na kuzifaidisha familia na uchumi kwa ujumla. Katika maeneo ya vijijini nchini China, mishahara iko juu sana kwa wale wanaojishughulisha na kazi zisizo za shamba na wenye angalau elimu zaidi ya sekondari.

Vijana wa vijijini wenye stadi za msingi wana uwezekano mkubwa wa kufanya kazi zisizo za shamba. Katika nchi nane zilizofanyiwa uchanganuzi katika Ripoti hii, kadri kiwango cha

Mchoro wa 16: Vijana wa kike wa vijijini wanakosa fursa zaidi ya kupata stadi za msingi

Asilimia ya vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24 ambao wako chini ya kiwango cha elimu ya kwanza ya sekondari, kwa kuzingatia jinsia, sehemu za vijijini za nchi zilizochaguliwa, miaka ya hivi karibuni




Chanzo: UIS (2012a).

elimu kinavyokuwa kikubwa, ndivyo kunavyokuwa na uwezekano wa kijana kupata ajira isiyo ya kilimo, vivyo hivyo kwa wanawake na wanaume. Nchini Uturuki, 23% ya wale wasio na elimu wanajishughulisha na kazi zisizo za kilimo, ukilinganisha na 40% ya wale wenye elimu ya msingi na 64% ya wale wenye elimu ya zaidi ya sekondari.

### *Kushughulikia mahitaji ya mafunzo vijijini*


Katika mipango ya taifa ya nchi arobaini na sita zilizofanyiwa uchanganuzi katika Ripoti hii, ni nusu tu zilitambua mahitaji ya mafunzo maalum na stadi ya maskini wa vijijini katika mipango yao ya taifa. Hata hivyo nchi zinazotoa kipaumbele kwa mahitaji ya maskini wa vijijini, zinaweza kufaidika. Nchi ya China, kutoka mwaka 1970, inatilia mkazo tija ya wakulima wadogo wadogo na ajira binafsi zisizo za kilimo ilipunguza idadi ya wale wanaoishi kwenye umaskini.

Kuhakikisha kwamba vijana wote wanapata stadi za msingi ni changamoto kubwa sana katika maeneo ya vijijini kwa sababu mtawanyiko wa watu na idadi ya wanaohusika. Hata hivyo, vijana katika maeneo ya vijijini hawatafaidikana mipango ya mafunzo kama wanakosa stadi za msingi ambazo zitawasaidia kuelewa na kutumia teknolojia mpya kwenye biashara na kilimo. Kupanua elimu rasmi ya msingi na sekondari na kuongeza uhalisia wake kwa mazingira ya vijijini ni vipaumbele vikubwa

Mkazo inabidi uwekwe kwenye mipango inayotoa fursa za pili ambayo inatoa stadi za msingi zikichanganywa namafunzo ya stadi zinazohusiana na kilimo na shughuli zisizo za kilimo kwa watu wa vijijini.

Nchini Malawi, ambapo 85% ya watu wanaishi maeneo ya vijijini, takribani nusu ya vijana wanaoanza shule elimu ya msingi huacha shule, mipango ya mafunzo inayotoa fursa za pili za kupata stadi, imekuwa na mafanikio makubwa sana. Ikiwalenga wale wanaoishi maeneo ya vijijini ambao hawajawahi kwenda shule au waliacha shule, ilipelekea zaidi ya nusu ya wanafunzi kumaliza kozi au kurudi shule ya msingi. Washiriki pia walipata matokeo mazuri kwenye kusoma na kuandika na kuhesabu kuliko wale walio kwenye mfumo rasmi wa elimu. Juhudi kama hizo zinahitajika katika nchi nyingi maskini zenye idadi kubwa ya watu wanaoishi vijijini na wenye elimu ndogo au wasio na elimu kabisa.

Mipango inabidi itatue matatizo maalum yanayowakabili wanawake wa vijana wa kike. Nchini Misri mwaka 2008, 20% ya wanawake wa vijijini wenye umri kati ya miaka 17 na 22 walisoma shule chini ya miaka miwili. Wengi wao wana uwezekano mkubwa wa kuolewa bado wadogo. Mpango wa Ishraq nchini Misri, unapambana moja kwa moja na dhana potofu za kijamii, kwa kufanya kazi familia, viongozi na jamii za vijijini, inawajumuisha ili kuonyesha mantiki ya mipango kutoa stadi za kujua kusoma na kuandika na kuhesabu kwa wasichana. Zaidi ya wahitimu tisa kati ya kumi wa kwanza wa mpango wa Ishraq walifaulu mitihani ya mwisho.




Kujumuisha mafunzo ya stadi za kusoma na kuandika na kuhesabu na stadi zingine kwenye mipango ya mikopo midogo midogo na hifadhi ya jamii kwa ajili ya wanawake maskini wa vijijini huongeza fursa zao za kutoka kwenye umaskini. Waanzilishi wawili wa mpango huu ni BRAC nchini Bangladeshi na Camfed huko Afrika. BRAC inawapatia familia maskini za vijijini rasilimali, kama ng'ombe, ili kuendesha maisha. Pia inawapatia mafunzo ya mikopo midogo midogo na utafutaji masoko ili kuongeza faida kwenye uwekezaji. Matokeo yake, kipato kwa kila mwana kaya kimeongezeka karibu mara tatu. Camfed inawalenga wasichana maskini wa vijijini, ikiwapa stadi za utawala wa biashara, ruzuku, mikopo midogo midogo na ushauri mwenzi. Mkakati wake umepelekea zaidi ya 90% ya biashara zilizoanzishwa na vijana wa kike kupata faida.

### *Kuwapatia vijana wa vijijini stadi za ziada*

Ili kuhakikisha kwamba kazi katika maeneo ya vijijini zinavutia vijana, ni muhimu kutoa mafunzo zaidi ya yale ya msingi ili wakulima wadogo wadogo waongeze tija kwenye kilimo na wafanyakazi wasio wakulima waboreshe stadi zao kwenye biashara na fedha.

Uanzishaji wa vyama unaweza kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kupata stadi wakati huo huo wakiimarisha sauti yao ya pamoja

Mashamba darasa na vyama vya ushirika ni mikakati miwili yenye mafanikio. Nchi Kenya, Uganda na Tanzania, mashamba darasa yamechangia uboreshaji mkubwa. Mkakati huu umekuwa wenye faida kwa wale wenye viwango vya chini cha elimu. Thamani ya mazao kwa ekari iliongezeka kwa wastani 32% katika nchi hizo tatu, na kwa 253% kwa wale wasio kuwa na elimu rasmi. Kipato kiliongezeka kwa wastani wa 61%, na kwa 224% kwa kaya ambazo kiongozi wake hakuwa kwenda shule.

Njia nzuri ya kuhimiza kujifunza kwenye tija na matumizi kwa vitendo ya stadi mpya ni kuzionyesha kupitia radio na video. Majaribio nchini Burkina Faso, India na Niger yameonyesha kuna faida kubwa ya kuongeze mafunzo kwa kutumia Teknohama, hususani radio ambayo inaweza kuwafikia idadi kubwa ya wakulima maskini.

Mipango bunifu ya mafunzo kwa kazi zisizo za kilimo inaweza kuwa na faida kubwa ya kuwatia moyo vijana kubaki maeneo ya vijijini. Mipango kadhaa yenye lengo la kuwapatia vijana maskini stadi za ujasiriamali na biashara ndogo ndogo, ikiwajumuisha vijana wenyeji, imeanzishwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya vijijini huko Amerika ya Kusini. Mingi kati ya hii imeonyesha matokeo ya kuvutia.

Nchini Mexico, mpango wa JERFT (Mpango wa Ujasiriamali na Ardhi kwa Vijana wa Vijijini) ulioanza mwaka 2004 ili kushughulikia ukosefu wa ardhi kwa vijana na hitaji la kizazi kipya cha wajasiriamali wa vijijini. Mpango ambao ulilenga makundi ya wenyeji, ulikuwa na lengo la kuwawezesha walengwa wake kuanzisha biashara za kilimo endelevu na zenye faida. Ndani ya mwaka mmoja, washiriki wake waliongeza kipato chao kwa asilimia ishirini.

Kama kilimo au sio, ni muhimu kwa mafunzo kuzingatia mazingira ya kila eneo husika, kwa kujaza mapengo ya wazi ya stadi katika eneo husika. Mafunzo kwa ajili ya Uwezeshaji Kiuchumi Vijijini (TREE) yaliyoandaliwa na ILO, yanafuata mkakati huu, yakisaidia kuhusianisha ugavi na hitaji la soko la ajira, yakichangia mafanikio makubwa katika mazingira tofauti katika mabara tofauti. Nchini Bangladeshi, yamewasaidia wanawake kuingia kwenye fani tofauti kama ukarabati wa vifaa na kompyuta. Mkakati huu unahusisha mafunzo ya ufundi na biashara pamoja na mafunzo ya masuala ya kijinsia na vipindi vya uelimishaji wa masuala ya kijinsia kwa familia, jamii na asasi washirika za wanafunzi.

# Stadi za vijana: Hatua za mstakabali wa maisha bora ya baadae





Kuna hitaji la haraka la kuchukua hatua ya kusaidia maendeleo ya stadi kwa vijana. Ripoti hii inaonyesha hatua kumi muhimu zinazopaswa kuchukuliwa. Hizi zinaweza kuandaliwa ili kuendana na mazingira na mahitaji maalum ya nchi

### 1 *Kutoa fursa ya pili ya elimu kwa wale wenye stadi za chini za msingi au kutokuwa nazo kabisa*

Kuwapa fursa ya pili ya elimu kwa vijana milioni 200 kwenye nchi maskini na za kipato cha kati ambao hawakumaliza elimu ya msingi kunahitaji mipango iliyoratibiwa vizuri na yenye fedha za kutosha katika eneo kubwa zaidi. Pamoja na misaada ya wahisani, serikali zinabidi zifanye suala hili kuwa la kipaumbele cha sera, likilijuimuisha kwenye mpango mkakati wa sekta ya elimu ambao unaweka malengo ya kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya vijana wasio na stadi za msingi. Mgawanyo wa bajeti unaozingatia idadi ya vijana maskini wanaohitaji fursa ya pili ya elimu inabidi uainishwe na kujumuishwa makadirio ya bajeti ya taifa.



### 2 *Kupambana na vikwazo vinavyozuia kujiunga na shule ya sekondari ya awali.*

Nchi zenye idadi kubwa ya vijana wanaokosa stadi za msingi zinahitaji kuanza kwa kupambana na vikwazo vinavyowazuia watoto na vijana maskini kushiriki na kuendelea kwenye elimu hadi walau kufikia kiwango cha sekondari ya awali. Kuondoa ada ya shule na kutoa msaada wa kifedha uliokusudiwa, kuunganisha elimu ya msingi na sekondari ya awali, kutoa mtaala mmoja ili kuwapatia watoto wote stadi za msingi, kuhakikisha kwamba kuna nafasi za kutosha kwenye shule za serikali na kuhakikisha kuna uwezekano wa kujiunga katika maeneo ya vijijini ni hatua muhimu ambazo zinaweza kuongeza uwezekano wa kupata elimu ya sekondari ya awali.

Lengo la kidunia inabidi liwekwe kuhakikisha vijana wote wanafaidika na elimu ya sekondari ya awali, ili kufikia lengo la elimu ya sekondari ya awali kwa wote yenye ubora unaokubalika ifikapo mwaka 2030. Mipango ya muda mrefu ya elimu inabidi iainishe mikakati na rasilimali fedha zinazohitajika kufikia lengo hili.

### 3 Kufanya elimu ya sekondari ya juu ipatikane zaidi kwa watu maskini na kuongeza uhusiano wake na kazi.

Elimu ya sekondari ya juu lazima iendane na mahitaji ya stadi kwenye soko la ajira. Kwanza inabidi iweke uwiano kati ya masomo ya ufundi na masomo ya kawaida kwa kutoa nafasi ya kuchagua masomo na kuhusianisha na sehemu za kazi.

Pili, mabadiliko ya mtaala wa elimu ya sekondari inabidi uwe mkazo zaidi kwenye kuongeza uwezo wa wanafunzi kutatua matatizo, na kutumia Teknohama kuwasaidia wanafunzi kuendeleza stadi zinazohitajika kwenye soko la ajira ambazo zinategemea sana teknolojia.

Tatu, fursa zinazoweza kubadilika inabidi zitolewe kwa wanafunzi ambao wako kwenye hatari ya kuacha shule ya sekondari. Vituo vya elimu ya masafa vinaweza kuanzishwa ili kukidhi mahitaji ya vijana maskini. Utambuzi stahiki inabidi utolewe kwa stadi zilizopatikana kupitia njia mbadala za kujifunza ambazo zinatoa fursa ya kurudi shule au zinatoa sifa kama za sekondari ambazo zinatambulika kwenye maeneo ya kazi.

**4 *Kuwapa vijana maskini wa mijini nafasi ya kupata mafunzo ya stadi ili kupata kazi nzuri***

Mikakati ya kitaifa inayotegemea mifumo ya iliyozoeleka ya mafunzo kwa vitendo inabidi iimarishe mafunzo ya mafundi wakuu, iboreshe mazingira ya kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba stadi zinaweza kuthibitishwa kupitia taratibu za kitaifa za utambuzi wa sifa. Pamoja na kuongeza uhalali wa mfumo uliozoeleka wa mafunzo kwa vitendo, hatua hizo zitahakikisha kwamba wanafikia viwango vya biashara na viwanda, na kuongeza uwezekano wa wanafunzi kupata kazi mbalimbali zenye malipo mazuri.

Mikakati inabidi itoe mafunzo ya stadi kwa vijana wanaopenda kuwa wajasiriamali, lakini isiishie hapo. Kuwapatia vijana fursa ya kupata fedha za kuanzishia biashara kunaweza kuwasaidia kutumia stadi zao kwa mafanikio.

**5 *Sera na mipango ilenge vijana wanaoishi kwenye maeneo maskini ya vijijini***

Vijana wengi wa vijijini wanahitaji kupewa fursa ya pili ya kupata stadi za msingi, pamoja na mafunzo ya mbinu za kilimo ambayo yanaweza kuwasaidia kuongeza tija. Mashamba darasa na mafunzo kupitia vyama vya ushirika, ambayo yanazingatia mahitaji ya wakulima wa eneo husika, yamekuwa na mafanikio. Kwa kuwa vijana wengi wa vijijini pia wanafanya kazi zisizo za shamba, mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa fedha yanaweza kuongeza fursa zao. Hii ni muhimu kwa sababu eneo la mashamba linazidi kuwa adimu na kutoa fursa ya kuwatia moyo vijana kubaki maeneo ya vijijini.

**6 *Kuhusianisha mafunzo ya stadi na hifadhi ya jamii kwa vijana maskini***

Kuunganisha mikopo midogo midogo au hifadhi ya jamii, kama uhamishaji wa rasilimali zenye tija, pamoja na mafunzo ya stadi za kusoma na kuandika na kuhesabu na kuendesha maisha imeonyesha kuwa na mafanikio kwenye kusaidia kupambana na aina mbalimbali za mazingira magumu ambayo yanaweza kuwafunga vijana kwenye umaskini.

**7 *Kutoa kipaumbele kwa mahitaji ya mafunzo kwa vijana wa kike wanaoishi kwenye mazingira magumu***

Mipango yenye malengo ambayo inashughulikia sababu mbalimbali za hali ngumu ambayo vijana wa kike wanakabiliana nayo imeonyesha kuwa na ufanisi. Kuwapa vijana wa kike mikopo midogo midogo na rasilimali za kuendesha maisha na ruzuku kwa ajili ya kuzalisha kipato, pamoja na stadi zinazohitajika ili kufaidika na rasilimali hizi, inawapa udhibiti mkubwa wa rasilimali zao katika namna ambayo inawafaidisha wao na familia zao.



© Jon Yamamoto/UNESCO

**8 *Kutumia uwezo wa teknolojia ili kuongeza fursa kwa vijana***

Teknohama inaweza kutumika kutoa stadi kwa idadi kubwa ya vijana. Hata teknolojia ya msingi kama radio inaweza kutoa mchango mkubwa kwenye mafunzo ya stadi, hususani kwa vijana wanaoishi kwenye maeneo mbali huko vijijini. Njia hizo zinabidi zitumiwe kikamilifu ili kuongeza fursa za mafunzo kwa vijana.

**9 *Kuboresha mipango kwa kuimarisha ukusanyaji wa takwimu na uratibu wa programu za kutoa stadi***

Uongozi wa serikali ni muhimu kwa kuratibu wadau mbalimbali na mafunzo ya stadi na programu zinazohusiana ili kuhakikisha kwamba zinaakisi vipaumbele vya taifa vinavyowalenga zaidi vijana maskini. Kwa kufanya hivyo kutapunguza ugawanyika na urudiaji wa mikakati, na kuhakikisha usawa kwenye kupata mafunzo.

Takwimu zaidi na zenye ubora zinahitajika na serikali na jumuiya ya kimataifa ili kufuatilia upatikanaji wa programu za kukuza stadi na hivyo kupanga kwa ufanisi zaidi. Ili kutoa taarifa kwa Taasisi ya Takwimu ya UNESCO taarifa bora zaidi kuhusu elimu ya sekondari ya awali na juu inahitajika. Hii inabidi ijumuishe taarifa zaidi za kuacha na kumaliza shule, na masomo yaliyosomwa, zikijumuisha maelezo kuhusu maeneo ya kitaaluma na ufundi, kusaidia uchanganuzi wa uchaguzi wa somo kulingana na jinsia.

Takwimu bora zaidi zinahitajika kuhusu mipango ya kukuza stadi zaidi ya mfumo rasmi wa elimu, kama programu za kutoa fursa ya pili na mifumo ya asili ya mafunzo kwa vitendo, kuunganisha takwimu hizi na taarifa za soko la ajira. Kutokana na utaalam wake katika eneo hili, ILO inaweza kubeba jukumu la kukusanya na kusambaza takwimu kutoka serikalini. Jumuiya ya kimataifa inabidi ijikite kwenye maendeleo ya karibuni ili kupima stadi mbalimbali za vijana na watu wazima kwa mpangilio mzuri zaidi.

Kuwashirikisha vijana hususani wale wanaokabiliana na mazingira magumu, kwenye kupanga ni muhimu ili kuainisha vikwazo na ufumbuzi stahiki. Serikali pia inabidi zifanye kazi kwa karibu na wafanyabiashara na vyama vya wafanyakazi ili kuongeza uhusiano kati ya mikakati ya mafunzo ya stadi na mahali pa kazi.



**10** ***Kukusanya fedha zaidi kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya mafunzo kwa vijana maskini***

Kuna hitaji la haraka, hususani katika nchi maskini, la rasilimali ili kuhakikisha kwamba vijana wote wana msingi mzuri wa elimu, na kuendelea walau hadi sekondari ya awali. Serikali na wafadhili watoe kipaumbele cha kutafuta fedha za ziada kwa ajili ya kusaidia mipango inayotoa fursa za pili kwa watu wengi zaidi. Kuhamishia kiasi cha dola bilioni 3.1 ambazo wafadhili wanatumia kwa ajili ya udhamini wa masomo na gharama za kusomesha wanafunzi kutoka nchi zinazoendelea kwenye nchi wafadhili zingesaidia kupatikana kwa dola bilioni 8 zinazohitajika kuhakikisha kwamba vijana wote wanamaliza elimu ya sekondari ya awali.

Sekta binafsi inaweza kuongeza msaada wake kwenye programu za kuendeleza stadi kwa vijana maskini kwa kupitia taasisi zao. Lakini inabidi msaada huo upatikane kwa watu wengi na uratibiwe kwa karibu pamoja na vipaumbele vya taifa.

Mifuko ya mafunzo ambayo inaleta pamoja rasilimali kutoka serikalini, misaada ya wafadhili na sekta binafsi imekuwa na mafinikio ya kuwafikia vijana maskini, ikiwemo wale walio kwenye sekta isiyo rasmi. Kuna uwezekano mkubwa kwa mifuko hii kukusanya fedha za ziada wakati zikiboresha uratibu miongoni mwa serikali, makampuni, wafadhili, vyama vya wafanyakazi, vikundi vya vijana na wadau wengine.

# VIJANA NA STADI
## Kuiweka elimu kwa vitendo

Toleo hili la kumi la Ripoti ya Ufuatiliaji wa Malengo ya Elimu kwa Wote Duniani linaonyesha kwamba ni muhimu kuhakikisha kwamba vijana wote wana stadi wanazohitaji ili kufanikiwa. Kama Ripoti inavyoonyesha, dunia nzima kuna kizazi kilichopotea cha vijana milioni 200 ambao wanamaliza shule bila kuwa na stadi wanazozihitaji. Wengi wanaishi kwenye umaskini maeneo ya mijini au jamii za pembezoni huko vijijini na hususani vijana wa kike, hawana ajira au wanafanya kazi kwa malipo kidogo. Wanahitaji kupewa fursa ya pili kutimiza ndoto zao.

Vijana na stadi : Kuiweka elimu kwenye vitendo inaelezea jinsi serikali zinavyoweza kuwapa vijana mwanzo mzuri kwenye maisha ili waingie kwenye ulimwengu wa ajira wakiwa wanajiamini. Pia inaainisha hali ya sasa ya kifedha kwa ajili kufikia malengo ya Elimu kwa Wote, ikionyesha majukumu ambayo serikali, wafadhili na sekta binafsi wanaweza kubeba ili kupata rasilimali mpya na kuzitumia kwa ufanisi zaidi.

Ripoti inafuatilia malengo sita ya Elimu kwa Wote katika zaidi ya nchi 200. Inaonyesha kwamba maendeleo bado yanasuasua na yanahitaji msukumo wa haraka ili kufikia malengo ifikapo mwaka 2015.

Uchanganuzi uliojikita kwenye ushahidi kwa ajili ya Ripoti hi ya Ufuatiliaji wa Malengo ya Elimu kwa Wote Duniani ni nyenzo muhimu kwa watunga sera za elimu, wataalamu wa maendeleo, watafiti, vyombo vya habari –na yeyote anayependa kutumia nguvu ya elimu ili kujenga dunia yenye ustawi na usawa.

*"(Kwenye mafunzo yangu kwa vitendo), nitaenda kwenye kituo ili kujifunza kukarabati kompyuta. Nikiwa najifunza kwenye kituo nitaweza kufanya mazoezi na baada ya kupata cheti nitaweza kupata kazi mara moja. Sitakuwa najifunza nadharia tu. Wataniruhusu kufanya mazoezi ya kuunganisha au kukarabati kompyuta."*

*-Kijana wa kiume kutoka Vietnam*

*"Nadhani italeta tofauti kubwa kama nitapata mtu mwenye elimu nzuri ili aniongoze na kunielewesha vizuri wito wangu. Kama mtu akinipa stadi na uwezekano wa kuanza kazi, najua naweza kutimiza malengo yangu."*

*-kijana wa kike kutoka Ethiopia*

*"Kwenye vyuo na shule, inabidi wafanye zaidi, na sio ruhusa ya siku moja ambapo unaenda kufanya mazoezi kidogo ya kazi, inabidi wawe na siku mbili shuleni na siku tatu sehemu ya kazi, ili kuweka uwiano. Kwa hiyo upo shuleni, unajifunza unachohitaji kujifunza na unatoka kwa ajili ya kupata uzoefu."*

*-kijana wa kike kutoka Uingereza*

*"Kuna ukosefu wa elimu hivyo hatuwezi kupata kazi na hatuwezi kuboresha maisha yetu. Hatuna maendeleo."*

*-kijana wa kiume kutoka India*

*"Ingawa sijamaliza masomo yangu nahitaji fursa. Tunataka kufanya kazi na kuchangia maendeleo ya nchi."*

*-Kijana wa kike kutoka Misri*

*"Kama nataka kuwa mtu mwenye maisha mazuri inabidi niendelee kusoma lakini kwa sababu za kiuchumi, siwezi kuendelea kusoma. Nilidhani ningeacha shule ili nisiwe mzigo na kulipia mahitaji yangu, lakini siwezi kupata kazi – je, ninawezaje kusoma?"*

*-Kijana wa kiume kutoka Mexico*

UNESCO
United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
UNESCO Publishing
EFA GMR EDUCATION FOR ALL GLOBAL MONITORING REPORT
www.unesco.org/publishing
www.efareport.unesco.org
9 789231 042409